**KORTI** yaamuru Selasini kumlipa Mbatia mil. 80/-

UKURASA 3



**HATIMAYE** DPP amalizana na Sabaya kesi ya uhujumu

UKURASA 3

**ACT** Wazalendo yahofia kuzidi kupanda bei za vyakula

UKURASA 4




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Mei 4, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581666

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Wanafunzi wafariki kwa kukosa hewa

## WALIKUWA wakitoa mahindi ghalani, Mkenda atoa tamko ..

*Endelea ukurasa wa 2*



Prof. Adolf Mkenda

## Maagizo 11 PM kuondoa vikwazo, mazingira wezeshi wanahabari

UKURASA 2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

## Mikoa yapewa hadhari athari kimbunga Hidaya

UKURASA 3

**MICHEZO** **MUSONDA, OKRAH WAIVURUGA YANGA** UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi (watano kulia), akiangalia athari za maafa baada ya tope na mawe kutoka mlimani kuporomoka na kusababisha vifo vya watu wanne katika Kijiji cha Lyakombila, Kata ya Kimochi, wilayani Moshi Vijijini, mkoani Kilimanjaro, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi wafariki kwa kukosa hewa

**Na Waandishi Wetu**

WANAFUNZI watatu wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari ya John Paul II, Kahama mkoani Shinyanga, wamepoteza maisha kwa kukosa hewa baada ya kuingia kwenye ghala la mahindi shuleni hapo.

Vifo hivyo vimeripotiwa ikiwa ni mwaka mmoja tangu kutokea kwa tukio la aina hiyo Mei 12, 2023 katika Shule ya Sekondari Kisomachi iliyoko Kata ya Vunjo Mashariki, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Kutokana na vifo hivyo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknlolojia, Prof. Adolf Mkenda, ametoa angalizo mahususi kwa walimu kuhusu usalama wa wanafunzi shuleni.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Kenedy Mgani, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo katika shule hiyo iliyoko Mtaa wa Mbulu, Kata ya Mhongolo wilayani Kahama, alipozungumza na waandishi wa habari jana.

Alisema vifo hivyo vilitokea Mei Mosi, mwaka huu, saa 5:00 asubuhi shuleni hapo walipoingia ndani ya ghala na baadaye kuzirai na kufariki dunia hatimaye kupelekwa katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama.

Kamanda Mgani aliwataja wanafunzi hao kuwa ni Abdul Ibrahim (17) mkazi wa Mwanza, Jonathan Mdabila (17) mkazi wa Nzega mkoani Tabora na Paul Emmanuel (18) mkazi wa Kahama. Alisema siku ya tukio, wanafunzi hao waliingizwa kwenye ghala, maarufu kama 'vihenge', lililojenga na mabati magumu kwa lengo la kutoa mahindi ya chakula cha siku hiyo.

Kamanda Mgani alisema walikuwa wanafunzi sita ambao waliongozana na mwalimu wa zamu, Moris Leo (54) kwenda kwenye ghala hilo na baada ya mahindi kushindwa kutoka kupitia tundu la chini ya tangi hilo, mwalimu huyo aliwataka wanafunzi kupanda juu na kuingia ndani kuyasukuma. Alisema baada ya kutoa agizo hilo, mwalimu huyo aliondoka eneo hilo na kwenda ofisini kupata chai, huku wanafunzi watatu kati ya sita, wakiingia ndani ya tangi hilo kwa kutumia ngazi.

Baada ya dakika kati ya 15 hadi 30, waliokuwa nje hawakuona mahindi yakitoka huku waliokuwa ndani wakiwa kimya, ndipo walipotoa taarifa kwa uongozi wa shule.

Alisema walimu walifika na kuangalia kinachoendelea na haraka wakachukua uamuzi wa kuvunja tangi hilo kwa shoka na kupata mpenyo wa kuwatoa na kuwapeleka katika zahanati ya jirani na shule na baadaye Hospitali ya Manispaa ya Kahama, ambako walipoteza maisha.

Mpaka sasa, alisema wanamshikilia mwalimu Leo kwa mahojiano zaidi na upelelezi unaendelea kuhusu tukio hilo.

**MKASA ULE ULE**

Mei, mwaka jana, kulitokea tukio kama hilo katika Shule ya Sekondari Kisomachi ambako wanafunzi wawili wa kidato cha mne walipoteza maisha katika mkasa unaofanana na huo. Nao walipanda katika tangi la kuhifadhia maharage.

Taarifa ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, siku hiyo ilisema tukio hilo lilitokea saa 10:00 jioni wakati wanafunzi hao walipoingia ndani ya tangi linalotumika kuhifadhia maharage kwa lengo la kuyatoa baada ya sehemu ya chini inayotumika kuziba.

Kamanda maigwa aliwataja wanafunzi waliofariki dunia ni Edson Mosha (17) na Godwin John (17).

**MKENDA ATOA ANGALIZO**

Baada ya kuripotiwa kwa tukio la Kahama, Nipashe ilimtafuta Waziri Mkenda ambaye alisema usalama wa watoto wote ni jambo moja la msingi na muhimu shuleni.

"Hatua zozote zinazochukuliwa hazina maana kama zitahatarisha usalama wao. Tuna jukumu la kuhakikisha tunaendesha shughuli na kulinda watoto tunaokabidhiwa shuleni. Tunafuatilia matukio yote mawili," alisema Prof. Mkenda.

Kimsingi wanafunzi waliofariki dunia ni watoto. Sheria ya Ulinzi wa Mtoto ya mwaka 2009, mbali na mambo mengine, inaelekeza watoto kupewa haki ikiwamo ulinzi wa usalama wao.

**IMEANDALIWA na Shaban Njia (KAHAMA) na Romana Mallya (DAR)**

# Maagizo 11 PM kuondoa vikwazo mazingira wezeshi wanahabari

**Na Paul Mabeja,**DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ametoa maagizo 11, ikiwamo viongozi na wakuu wa taasisi zote kuondoa vikwazo vya utoaji taarifa kwa vyombo vya habari na kuweka mazingira wezeshi kwa wanahabari ili kuwarahisishia utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Majaliwa alitoa maagizo hayo jana jiji hapa, alipokuwa akizungumza kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani.

Alisema wakuu wa taasisi wanapaswa kuondoa ukiritimba uliopo kwenye utoaji wa taarifa ili kuwezesha vyombo vya habari kutoa taarifa kwa wananchi.

"Wakuu wa taasisi wote ondoeni ukiritimba wa utoaji wa habari kwa waandishi wa habari ili kuwezesha kupatikana kwa habari zenye viwango zinazohitajika na wananchi wetu lakini pia wekeni mazingira wezeshi na rafiki kwa wanahabari kupata habari," alisema Majaliwa

Pia alisema usalama kwa waandishi wa habari wakati wa utekelezaji wa majuku yao ni jambo na muhimu, hivyo serikali itaendelea kusimamia kwa karibu jambo hilo.

"Serikali itaendelea kusimamia suala la usalama wa waandishi wa habari ili kuhakikisha kuwa hakuna mwandishi wa habari hata mmoja anapata shida wakati wa utekelezaji wa majukumu yake," alisema

Waziri Mkuu pia aliagiza maofisa wote wa serikali ambao wamekuwa na jukumu la kuratibu ziara za viongozi wa serikali, kuhakikisha waandishi wa habari wanakuwa na usafiri wa uhakika ili wasipate tabu kutekeleza majukumu yao.

Pia alisema kutokana na athari kubwa za mabadiliko ya tabianchi duniani, vyombo vya habari vinapaswa kutumia nafasi yao kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira.

"Tunalo jukumu la kuelimisha umma kuhusu utunzaji wa mazingira. Tunavyo vyombo vingi lakini vingi haviandiki habari zinazohusu mazingira, hivyo kupitia majadiliano yenu, inabidi muone ni kwa namna gani habari za mazingira zinapewa uzito mkubwa ili kulinda mazingira," alisema.

Alisema utafiti unaonyesha takribani watu milioni 16 nchini wanaoishi pembezoni mwa bahari, hivyo maisha yao yanategemea rasilimali za baharini kwa hiyo kama mazingira yataharibiwa, maisha yao yatakuwa hatarini.

"Lakini uharibifu wa mazingira unachangia kuongezeka kwa joto, magonjwa na takwimu zinasema kuwa asilimia 50 ya Watanzania bado wanatumia kuni na asilimia 20 wanatumia mkaa, hivyo lazima tuunge mkono juhudi za serikali kuhamasisha matumizi ya nishati safi," alisema.

Mkurugenzi wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Kenneth Simbaya, alisema katika maadhimisho ya mwaka huu, wamejadiliana mambo mbalimbali ikiwamo waandishi wa habari kuzingatia maadili.

Simbaya pia alisema waandishi wahabari wanapaswa kutoa taarifa katika vyombo husika kila wanapokutana na vitendo vinavyo tishia usalama wao wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao ili hatua zichukuliwe.



Rais wa Zanzibar, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na waumini wa Dini ya Kiislamu, baada ya Sala ya Ijumaa katika Msikiti wa Mchangani, Wilaya ya Mjini Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Mikoa yahadharishwa athari kimbunga 'Hidaya'

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imeagiza mamlaka za mikoa zitakazokumbwa na athari za kimbunga cha Hidaya kuendelea kuchukua tahadhari za kutosha ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kuhusu mwenendo wake, ili hatua stahiki zichukuliwe iwapo dalili zilizobainishwa zikijitokeza.

Tahadhari hiyo imetolewa baada ya kasi ya kimbunga hicho kuendelea kusogea Pwani ya Tanzania, huku kikitarajiwa kuendelea mpaka Mei 6, mwaka huu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama, alitoa tahadhari hiyo jana bungeni jijini Dodoma.

Mhagama alisema kwa mujibu wa taarifa iliyotewa jana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), kimbunga hicho ambacho kinachokuja uelekeo wa Mashariki mwa Pwani ya Tanzania, kimeendelea kuimarika na kusogea eneo la pwani mwa Tanzania.

Alisema hadi kufikia saa tisa usiku jana, kilikuwa kimeimarika zaidi na kufikia hadhi ya kimbunga kamili kikiwa umbali wa km 401 Mashariki mwa Pwani ya Mtwara.

Waziri Mhagama alizitaka taasisi mbalimbali nchini zikiwamo kamati za usimamizi wa maafa ngazi za mikoa, wilaya, kata, mitaa na vijiji kuendelea kuchukua tahadhari na kufuatilia kwa karibu taarifa za mamlaka ya hali ya hewa.

"Wananchi wanaoishi katika maeneo yaliyotajwa na wote wanaojihusisha hasa na shughuli mbambali baharini, wanashauriwa kuchukua tahadhari kubwa ikiwa ni pamoja na kuendelea kufuatilia taarifa za utabiri kutoka mamlaka husika," alisisitiza.

Mhagama alisema katika kipindi hiki, kimbunga Hidaya kimeendelea kuimarika zaidi huku kasi ya upepo ikiongezeka hadi kufikia kilometa 130 kwa saa na mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa baharini bado inaonyesha uwezekano mkubwa wa kimbuka kusalia katika hadhi ya kimbunga kamili hadi kufikia saa 12 zijazo huku kikiimarika.

Alisema kibunga hicho kitaendelea kusogea kabisa katika Pwani ya Tanzania ambapo kinatarajiwa kuendelea kuwapo hadi Mei 6, mwaka huu, na kupungua nguvu baada ya tarehe hiyo.

Kuwapo wa kimbunga hicho nchini, alisema kunatarajiwa kutawaliwa na kuathiri mifumo ya hali ya hewa ikiwa ni pamoja na kuathiri vipindi vya mvua kubwa na upepo mkali katika baadhi ya maeneo ya mikoa.

Mhagama aliitaja mikoa hiyo ni Mtwara, Lindi, Pwani pamoja na Visiwa vya Mafia, Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na upande wa pili wa muunga katika maeneo ya Unguja na Pemba.

Alisema kutakuwapo kwa vipindi vya mvua nyepesi na upepo wa wastani ambavyo tayari vimeanza kujitokeza katika maeneo ya Mtwara, huku ongezeko la mvua na upepo mkali unaoambatana na mawimbi makubwa, vikitarajiwa kusambaa katika maeneo mengi ya ukanda wa pwani kuelekea leo hadi Jumatatu ijayo (Mei 6, mwaka huu).

Pia aliziomba taasisi za dini, viongozi pamoja na wananchi kuendelea kumuomba Mungu kadri ya imani zao ili ikiwezeka nchi iepukane na janga hilo hatari.

"Mamlaka ya Hali ya Hewa inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa kimbunga Hidaya pamoja na athari zake kwa mifumo ya hali ya hewa hapa nchini na itaendelea kutoa taarifa kila baada ya masaa matatu, mara kwa mara pale itakapobidi," alisema.

Baadaye, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma, Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alisema kasi ya kimbunga hicho hadi jana jioni iliongeza hadi kufikia km 342 kutoka Pwani ya Mtwara.

# Korti yaamuru Selasini kumlipa Mbatia mil. 80/-

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imemtaka Makamu Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, Joseph Selasini, kumlipa fidia ya Sh. milioni 80 aliyekuwa mwenyekiti wa chama hicho, James Mbatia.

Selasini ametakiwa kumlipa fidia hiyo Mbatia kutokana na kumchafua kuwa aliwaomba rushwa Suzan Masele na Joyce Sokombi ili wateuliwe wabunge wa viti maalum.

Mahakama hiyo ilifikia uamuzi huo baada ya kujiridhisha kwamba maneno aliyoyatoa Selasini yalikuwa ya udhalilishaji na pia imemtaka ama aende Musoma alikotoa maneno hayo au kuomba radhi kwenye gazeti linalosambazwa eneo kubwa la nchi katika ukurasa wa mbele.

Uamuzi huo ulitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu, Aaron Lyamuya, katika Shauri la Madai Na. 87/2023 lililofunguliwa na Mbatia dhidi ya Selasini, akimtaka amlipe fidia ya Sh. milioni 500 kwa kumchafua.

Hakimu Lyamuya alisema mahakama imejiridhisha kwamba maneno aliyoyatamka Selesani yalikuwa ya udhalilishaji kwa kuwa yalikuwa yana viashiria vya jinai kwa sababu yalikuwa yanahusisha tuhuma za rushwa.

Kutokana na kujiridhisha huko, alimwamuru Selasini aombe radhi kwa njia mbili, ama arudi Musoma alikofanyia kikao cha kumchafua ili aombe radhi au aombe radhi kwenye gazeti lolote linalosambazwa eneo kubwa la nchi ukurasa wa mbele na kumlipa amlipe Sh milioni 80 fidia kwa kumdhalilisha.

Pia mahakama hiyo imetoa zuio kwa Selasini au mtu yeyote kutoa maneno ya udhalilishaji dhidi yake na pia Selasini anatakiwa kulipa gharama za shauri hilo.

Ilidaiwa kuwa maneno hayo ya udhalilishaji, Selasini aliyoyatoa katika kikao kilichofanyika nyumbani kwa Mzee Chimera eneo la Mlango Mmoja, Kata ya Nyasho mkoani Mara.

Alidai kwamba Mbatia alipokea fedha kutoka kwa Susan Masele Sh. milioni 70 na Joyce Sokombi Sh. milioni 30 ili kuteuliwa wabunge wa viti maalum.

Katika maombi yake, Mbatia aliiomba mahakama kwamba Selasini amwombe radhi kwa kumchafua, alipwe fidia ya Sh. milioni 500 na itoe amri ya zuio kwa mtu yeyote au kwa Selesini kuendelea kumchafua. Pia aliomba gharama za kesi alipe mlalamikiwa (Selasini).

# DPP amalizana na Ole Sabaya kesi ya uhujumu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SAA moja lilitosha jana kuafikiana na kutamatisha rufani namba 155 ya Kesi ya Uhujumu Uchumi Na. 27 iliyokuwa inamkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai,mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, na wenzake sita katika Mahakama Kuu ya Tanzania , Kanda ya Arusha.

Mazungumzo hayo yalikuwa kati ya mawakili wa serikali na wale wanaomtetea Sabaya.

Baada ya majadiliano hayo ya pande mbili, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), aliiandikia mahakama hiyo barua rasmi ya kutokuwa na nia ya kuendelea na rufani kisha kuiondoa mahakamani.

Katika rufani hiyo, mleta rufani alikuwa DPP na wajibu rufani ni Ole Sabaya na wenzake, Sylvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), John Odemba, Jackson Macha(29) na Nathan Msuya (31).

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya viwanja vya mahakama, Wakili wa Sabaya, Mosses Mahuna, alisema rufani ilikwenda kwa ajili ya kusikilizwa kabla ya wao kupeleka maombi Mahakama ya Rufani kuomba ifanye mapitio na marejeo ya mwenendo wa usikilizaji wa kesi hiyo kwa kuwa hawakuridhika nao.

"Baada ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania kufanya marejeo na mapitio ya namna shauri lilivyokuwa likiendeshwa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, iliamua kufuta mwenendo mzima na kuamua rufani hii kuanza kuendelea kusikilizawa upya.

"Leo (jana) rufani hii imeitwa kwa ajili ya kusikilizwa baada ya uamuzi ule wa Mahakama ya Rufani wa kubatilisha mwenendo ambao ulikuwa umeanza kusikiliza awali," alieleza Mahuna.

Wakili Mahuna alisema baada ya kufika mahakamani kwa lengo la kusikilizwa kwa rufani DPP, aliwasilisha notisi ya kuifahamisha mahakama kuwa, hana nia ya kuendelea na rufani hiyo.

"Mahakama baada ya kupokea notisi ya DPP, imefuta rufani hii rasmi leo (jana) mbele ya mahakama, hivyo Sabaya hana tena kesi inayomkabili kwa kuwa, zote zimekwisha malizika,"alieleza Mahuna.

Juni 4, 2021, Sabaya na wenzake walifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza na kusomewa mashtaka matano yaliyokuwa yakiwakabili katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza lilikuwa kuongoza genge la uhalifu kinyume cha Sheria ya Uhujumu Uchumi Kifungu cha 57(1) na 60(2).

Shtaka la pili lilikuwa la kujihusisha na vitendo vya rushwa na lilikuwa linamkabili Sabaya pekee na ilidaiwa ni kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Kifungu cha 15(1B,2) Sura ya 329, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.




Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (kulia), akitembelea maonyesho wakati wa mkutano Mkuu wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani Tanzania (APHYTA), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# ACT yahofia kupanda bei za vyakula

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI Kivuli wa Kilimo, Umwagiliaji na Maendeleo ya Ushirika wa Chama cha ACT-Wazalendo, Mtutura Abdallah, amesema endapo bajeti ya kilimo haitaongezwa kwa mwaka wa fedha 2024/25, bei za vyakula zinaendelea kupanda na kuathiri maisha ya watanzania.

Abdallah aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati chama hicho kikichambua bajeti ya kilimo iliyowasilishwa bungeni juzi.

Alisema bajeti ya kilimo isipoongezwa hususani kuiwezesha Wakala wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kununua na kuhifadhi chakula cha kutosha, bei ya vyakula itapanda.

"Bado miradi mingi ya umwagiliaji ipo katika hatua ya ndoto na hata iliyokwisha kuanza, kutekelezwa wake ni sawa na mwendo wa konokono," alisema. Abdallah alisema Tanzania inaendelea kutegemea sekta ya kilimo katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi wake kwa kutoa ajira kwa asilimia 61.1 ya nguvu kazi, na inachangia zaidi ya asilimia 100 ya chakula kinachopatikana nchini.

Alisema mpango wa bajeti unapaswa kubeba dhima hiyo ya kukabiliana na changamoto za uzalishaji, uhifadhi na mauzo ya chakula.

"Wanatakiwa kuhakikisha wakulima wanapata kwa wakati pembejeo za kilimo kwa kuwekeza ruzuku, ili kuwawezesha kumudu gharama na kuongeza tija katika uzalishaji,"alisema.

Alisema mikakati ya kilimo lazima ifungamanishwe na viwanda ili kuongeza thamani, kuongeza uzalishaji na kuhakikisha kunakuwa na masoko ya uhakika ya bidhaa za mauzo ndani ya nchini na ziada kusafirishwa nje.

Abdallah aliihatarisha serikali kuruhusu mbegu za GMO kuwa ni kusababisha kifo cha mbegu na chakula asili ambazo ndiyo tegemezi kwa wakulima wadogo vijijini ambao hawataweza kumudu gharama za kununua mbegu za GMO kila msimu wa kilimo.

Aidha, aliitaka serikali itoe tamko la kusitisha msimamo wake wa kutokuendelea na utafiti unahusiana na mbegu za GMO, na ihakikishe wakulima wa Tanzania wanalindwa dhidi ya mbegu hatari zitakapoanza kutumika kwa kuwa, katika nchi za jirani wamesikia zikiruhusiwa.

"Matumizi ya mbegu za GMO zimekuwa zikipingwa katika nchi nyingine hata za Ulaya, ambapo matumizi yake yalianza. Serikali ihakikishe sekta ya kilimo inafanya mageuzi yatakayowalinda wakulima wadogo," alisema.

Alisema mfumo wa stakabadhi ghalani umekuwa ni kitanzi kwa wakulima na kuwaachia maumivu makubwa, badala ya kuwa msaada kama ambavyo ilitarajiwa.

Abdalah alisema changamoto ya mfumo huo, hakuna ushirikishwaji wa moja kwa moja kuhusu kuamua bei ya mazao ya wakulima, na ucheleweshaji wa malipo kwa wakulima, jambo ambalo wakulima wengi hawawezi kumudu na kujikuta wakiuza kwa watu wa kati.

"Tumeangalia bajeti na vipaumbele vyake vya wizara, hatujaona mkakati wa kuboresha mfumo huo, ili kuwezesha na kuwanufaisha wakulima, tunataka huu mfumo uimarishwe uwe wa kieletroniki na uwe wa papo kwa papo,".

Abdalah aliitaka serikali kueleza fedha za ruzuku zimepelekwa wapi, ikiwa wakulima hawajanufaika nayo.

Alisema ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), inaonyesha wakulima milioni 2.55 kati ya milioni 3.4, waliosajiliwa katika mpango wa ruzuku sawa na asilimia 75, hawakupata wala kutumia mbolea kupitia mpango wa ruzuku, licha ya kuwa na sifa ya kupatiwa mbolea hiyo ya ruzuku.

Alisema ACT inaitaka serikali kuingilia kati mfumo wa uagizaji na usambazaji kwa kuiwezesha kibajeti kampuni ya taifa ya Mbolea (TFC), kuagiza nje na kusambaza mbolea nchini, ili kuongeza uwezo wa usambazaji wa mbolea unaotokana na kulegalega.

Abdallah alisema wanachokitaka ni serikali irejeshe mfumo wa uagizaji wa mbolea, kulipa madeni ya wasambazaji wa mbolea na kuondoa utegemezi wa mbolea kutoka nje ya nchi kwa kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji ili watu kujenga viwanda.

# Waziri atangaza Tanzania kitovu utalii tiba

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema imedhamiria kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi katika Bara la Afrika na kuwa nchi ya kutembelewa kwa ajili ya utalii tiba kutokana na uboreshanji wa miundombinu ya afya maeneo yote nchini. Hayo yalisemwa jana Dar es Salaam na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alipokuwa akifungua mkutano Mkuu wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani Tanzania (APHYTA).

Alisema huduma za kibobezi zitakazoimarishwa na kuvutia utalii tiba ni upandikizaji figo, upandikizaji uloto kwa wagonjwa wenye magonjwa ya damu kama Siko seli na Leukemia na utoaji wa uvimbe kwenye sakafu ya fuvu bila kufungua kichwa.

"Huduma nyingine ambazo tunaimarisha ni za kiuchunguzi wa kibingwa na kuwepo kwa madaktari bingwa bobezi kunakoifanya Tanzania kuwa nchi yenye kuvutia katika eneo la tiba utalii.

"Madaktari bingwa wa magonjwa ya ndani wanayo nafasi kubwa katika kusaidia kuboresha huduma za kliniki za magonjwa ya ndani na hivyo kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi. Ni imani yangu kuwa, endapo tutaendelea kutoa huduma zilizo bora na kuitangaza nchi yetu nje ya mipaka itasaidia kuimarisha tiba utalii," alisema.

Ili kufanikisha hilo, alisema serikali itawaendeleza kitaaluma madaktari bingwa kupitia programu maalumu ijulikanayo kama Dkt. Samia Super-Specialized Scholarship Programme.

Alisema tayari programu hiyo imetoa nafasi za ufadhili wa masomo ya ubingwa ambapo kwa mwaka wa Masomo 2023/24, kiasi cha Sh. 10.9 bilioni zimetengwa na kuwawezesha wanafunzi 1,109 kwenye masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 582 sawa na asilimia 110 ukilinganisha na mwaka wa masomo wa 2022/23. Aidha, alisema mipango mingine ya Wizara yake ni kuhakikisha kuwa hospitali zote za rufani za mikoa zinatoa huduma za kibingwa katika huduma za fani nane za kitabibu.

# Wasisitizwa kuhama maeneo hatarishi

**Na Maulid Mmbaga**

WANANCHI wamehimizwa kuendelea kuchukua tahadhari na kuondoka katika maeneo hatarishi yenye viashiria vya kuathiriwa na maafa ili kulinda usalama wao hasa katika kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha katika mikoa mbalimbali nchini.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu Dk. Jim Yonazi, wakati wa ziara yake ya kukagua baadhi ya maeneo yaliyoathiriwa na maafa ya mafuriko yaliyotokea Aprili 25, mwaka huu, katika mkoa wa Kilimanjaro katika kata za Msaranga, Mji Mpya na Kisomochi.

Dk. Yonazi alisisitiza wananchi kuzingatia taarifa zinazotolewa na serikali pamoja na kuendelea kuchukua tahadhari za mapema ili kuendelea kujilinda na kuwa na jamii stahimilivu dhidi ya maafa.

"Serikali itaendelea kukabiliana na maafa mbalimbali nchini kwa kuendelea kutoa elimu juu ya namna ya kujiandaa na kukabili maafa ili kuondokana na madhara yatokanayo na maafa pindi yanapotokea," alisema Dk. Yonazi.

Alifafanua kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo yenye dhamana ya masuala ya menejimenti ya maafa hivyo itaendelea kuratibu kwa weledi na kuyafikia malengo kama inavyotakiwa.

Pia alihimiza uongozi wa mkoa huo kuendeleza juhudi katika kuelimisha umma kuhusu masuala ya maafa pamoja na kuwatumia wataalamu wa masuala ya Ustawi wa Jamii kutoa huduma za kisaikolojia kwa waathirika wa maafa hayo ili kuondokana na madhara waliyoyapata na kurejea katika shughuli zao za kila siku.

"Tutaendelea kushirikiana na mkoa wa Kilimanjaro ili kuona hatua bora za urejeshaji wa hali na kipekee niendeleee kuupongeza uongozi wa mkoa huu kwa hatua mlizochukua toka maafa yalipotokea niwasihi kuongeza nguvu katika utoaji wa elimu ya majanga na maafa," alisisitiza.

Akitoa taarifa ya hali ya maafa, Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi, Mwajuma Nasombe, alisema maafa hayo ya mafuriko yaliathiri kata mbili ikiwemo ya Saranga na Mji Mpya na kusababisha athari kwa kaya 283 zenye jumla ya watu 1195.

"Jumla ya nyumba 51 na kifo cha mkazi mmoja kilitokea katika maeneo ya Mji Mpya ambako nyumba 35 zilibomoka kuta, 15 kuvyunjwa na maji pamoja na nyumba moja kubomoka kabisa," alisema.

Nasombe alisema serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kufanya tathimini ya kujua maeneo yaliyoathirika, kutoa huduma na misaada ya kibinadamu, kutenga maeneo maalum ya kuwahifadhi ili kuwapatia mahitaji waathiriki wa maafa hayo.

Naye, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Tixon Nzunda, alisema kata hizo zilizoathiriwa na mafuriko hayo huduma za msingi zimeendelea kutolewa ikiwemo misaada ya kibinadamu lengo kuwasaidia kuendelea kuwa na unafuu kutokana na madhara waliyopata.

HABARI KITAIFA

# Mafundi ujenzi, mkulima mbaroni madai ya mauaji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani hapa linawashikilia watu watatu wakiwamo mafundi ujenzi kwa tuhuma za mauaji ya mfanyakazi wa ndani, Monica Paul (22), mkazi wa Mtaa wa Lukuyu, Kata ya Bigwa, katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Mtuhumiwa mwingine, Rehema Omary (30), mkulima na mkazi wa Mwembesongo, anadaiwa kukutwa na simu ndogo ya marehemu aina ya Tecno.

Inadaiwa watuhumiwa hao walitekeleza mauaji hayo katika nyumba iliyoko Lukuyu-Bigwa baada ya kufika na kuanza kuiba vitu, mfanyakazi huyo katika kutetea ndipo walipomuua.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama, alisema tukio hilo lilitokea Aprili 14, mwaka huu, usiku ambapo watuhumiwa wawili ambao ni mafundi ujenzi walikuwa wakitumiwa na mmiliki wa nyumba hiyo aishie Dar es Salaam, kufanya matengenezo nyumbani hapo.

Aliwataja mafundi hao ni Mbaraka Omary (25), mkazi wa Tubuyu, ambaye amekutwa na vielelezo TV aina ya Hisence inchi 60, redio sabufa aina ya Boss, spika ndogo za redio hiyo na feni nyeupe ndogo aina ya Easy Home ambavyo vyote viliibiwa siku ya tukio.

Kamanda alimtaja fundi mwingine kuwa ni Mussa Mrisho (23), mkazi wa Bigwa, ambaye anadaiwa alishirikiana na mwenzake kutekeleza mauaji hayo, wakati mtuhumiwa Rehema Omary (30), mkulima, mkazi wa Mwembesongo, alikutwa na simu ndogo ya marehemu aina ya Tecno.

"Hawa mafundi walitumia mwanya huo wakitambua binti huyo ni dhaifu alikuwa peke yake na baada ya kufanya mazoea, Aprili 14, mwaka huu, walikwenda hapo nyumbani usiku kufanya tukio la mauaji yake," alisema.

Alisema watuhumiwa walifika usiku na kumgongea mlango mfanyakazi huyo naye alifungua kwa kuwa ni watu ambao anawafahamu, alipofungua wakaanza kuiba mali zilizokuwamo ndani, na wakati wa kunyang'anyana ndipo tukio la kumuua likafanyika. Kutokana na tukio hilo, Kamanda Mkama alitoa tahadhari kwa wananchi kutumia mafundi ujenzi wanaofahamika ili kuepusha vitendo vya kihalifu, huku akiwaomba wananchi kutoa taarifa za wahalifu ili zifanyiwe.

# Wabunge wataka bei elekezi ununuzi mazao kwa wakulima

**Na Vitus Audax,** DODOMA



Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Jacqueline Msongozi,



Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Sophia Mwakagenda,

SERIKALI imeombwa kuja na mpango mkakati wa kuweka na kusimamia utekelezaji wa bei elekezi za kununua mazao kutoka kwa wakulima ili kuokoa uchumi wao hususani kahawa na mahindi yanayouzwa kwa hasara na kutofautiana baadhi ya maeneo.

Wakichangia hoja katika makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2024/25, baadhi ya wabunge walisema, licha ya mazao yao kuwa na thamani kubwa yamekuwa yakinunuliwa kwa bei ya hasara kutoka kwa wakulima.

Kuhusu mahindi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Jacqueline Msongozi, alisema zao hilo limekuwa tofauti katika maeneo mbalimbali hususan katika kipindi cha mavuno na kusababisha hasara wakulima kutokana na kununua pembejeo kwa bei elekezi ambayo ni moja katika maeneo yote.

Alitoa mfano katika maeneo ya Songwe ambako alisema zao hilo linanunuliwa kutoka kwa wakulima kupitia bei iliyowekwa na Wakala wa Taifa wa Kuhifadhi Chakula (NFRA) ya Sh.1,000 kwa kilo moja, huku Ruvuma ikiwa ni Sh. 750. "Wote wanawekewa ruzuku katika mbolea, pembejeo zinaletwa kwa bei sawa, sasa kwa nini maeneo mengine yanunuliwe kwa bei juu na kwingine chini, weka uwiano wa ununuzi inaweza kuwa tofauti, lakini isiwe kubwa kama ilivyo sasa," alisema.

Mbunge wa Moshi Vijijini (CCM), Prof. Patrick Ndakidemi, alisema bei ambayo hahawa inanunuliwa kutoka kwa mkulima ni ndogo kuliko soko la kahawa lilivyo duniani.

Alisema kahawa ni zao maarufu duniani likishika nafasi ya pili na ina wakulima zaidi ya milioni 25 Tanzania ikiwa miongoni ambao ni wadogowadogo wanaozalisha asilimia 80 ya zao hilo duniani, licha ya kuwa na maisha magumu.

"Bei wanazopata ni ndogo kulinganisha na thamani ya zao lenyewe, na hazitoshelezi kulingana na kazi kubwa ya uandaaji wa zao hilo. Maana kwa kahawa aina ya Robusta kilo moja ni Sh. 2,000, huku Arabica ikiwa ni Sh.3000," alisema.

Mbunge Ndekidemi alisema kilo hiyo inayouzwa kwa bei hiyo ikienda nje inazalisha vikombe 120 hadi 140 vya kahawa, huku bei ya kikombe kimoja cha kahawa, ikiwa ni Dola za Marekani 3.5 hadi 3.7 sawa na Sh. 8,750 hadi 9,300 kwa kilo moja (sawa na zaidi ya Sh. milioni 1.05 hadi 1.3).

"Kwa hiyo hapa inaonekana kuwa, bei ya mkulima anayouza kilo moja ya kahawa ni sawa sehemu kidogo ya kikombe kimoja cha kahawa anayoiuza," alifanua.

Mbunge huyo aliishauri serikali kusaidia wananchi kupata masoko ya uhakika wa zao hilo na siyo kuendelea kuuza kwa bei ya hasara, ili kukabiliana na ukiritimba unaoendelea.

Aliitaka serikali iwashawishi wawekezaji wa uhakika kuja kuwekeza nchini viwanda vya uchakataji wa zao hilo ili kuuza bidhaa zilizochakatwa.

Mbunge wa Muleba Kasikazini (CCM), Charles Mwijage, aliishauri serikali kubaini na kutunza maeneo ya uzalishaji wa mazao muhimu nchini ikiwamo kahawa na zababu ili yasiathiriwe na maendeleo pamoja na ukuaji wa kidemgraphia.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, alisema wakulima wa parachichi wilayani Lungwe pamoja na maeneo mengine wanadhurumiwa haki zao kupitia mizani inayotumiwa na madalali wakati wa manunuzi ya zao hilo.

Aliitaka serikali kuingilia kati suala hilo na kuanza kwenda kwa wakulima na kupima na kununua yenyewe mazao hayo na kuacha kuwatumia madalali hao ambao wanawaumiza.

"Mizani inayotumika ununuzi mazao kutoka kwa wakulima itazamwe na kurekebishwa, kwani wakulima wanatoka kwenye maeneo yao wakiwa wamepima vyema mazao yao, wakifika kwa wanunuzi vipimo vinapungua kwa kilo kuanzia tano, hali ambayo inazidi kuwaumiza," Mbunge Viti Maalum (CCM), Bupe Mwakang'ata alisema.

twiga cement
Heidelberg Materials

Tanzania Portland Cement Public Limited Company
P.O.Box 1950,Dar es Salaam-Tanzania
Telephone:+255 746 810930
Fax: +255 746 810931
www.twigacement.com

**TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY NOTIFICATION TO THE PUBLIC**

This is to notify the generalpublic, and specifically shareholders of Tanzania Portland Cement Public Limited Company that the directors of the company propose a dividend of TZS 390 per share relating to the financial year ended 31st December 2023, which will be paid on or about **30th June 2024.**

For purposes of this dividend payment, the Register of Members will be closed on **28th May 2024,** and the last day of trading cum dividend will be on **22nd May 2024.**

**BY ORDER OF THE BOARD**

Alfonso Velez
For: Chairman of the Board
2 May 2024

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maboresho viwanja Ligi Kuu yaende sambamba na usajili

WAKATI msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara mwaka 2023/204 unaelekea ukingoni, tayari klabu zimeshaanza maandalizi mengine kwa ajili ya msimu mpya wa mashindano.

Kwa mujibu wa kalenda iliyotolewa na Bodi ya Ligi (TPLB), iliyopewa baraka na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara unatarajiwa kumalizika ifikapo Mei 28, mwaka huu.

Timu zote 16 zinazoshiriki ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Biashara ya Taifa (NBC), zitashuka katika viwanja nane tofauti nchini kucheza mechi za kufunga pazia.

Huku tayari Yanga, ambao ni mabingwa watetezi wakionekana wako katika nafasi nzuri ya kutetea taji wanalolishikilia, lolote linaweza kutokea kwa timu ambazo ziko katika hatari ya kushuka daraja, hii inatokana na kuwapo kwa tofauti ndogo ya pointi.

Timu nne kati ya saba ambazo ziko katika nafasi za chini kwenye msimamo, zinaweza kukutaka na janga hilo endapo hazitacheza vyema karata zake kwenye michezo iliyobakia ya lala salama, ikiwamo Mtibwa Sugar ambayo kwa sasa inaburuza mkia.

Kama ilivyo desturi, kila timu inafanya maandalizi yake kulingana na uwezo pamoja na kutaka kufikia malengo ya klabu husika.

Ni vizuri timu kuanza maandalizi mapema kwa ajili ya kuboresha vikosi vyao pamoja na kuongeza nguvu katika mabenchi ya ufundi, wakidhamiria kusaka matokeo chanya kwenye mechi za mashindano yote wanayoshiriki.

Kumekuwa na mazoea ya timu kusahau kutengeneza au kufanya maboresho ya viwanja ambavyo wanatarajia kuvitumia katika msimu mpya wa kupelekea kubadilisha vituo kutokana na viwanja walivyotarajia kufungiwa kwa sababu ya kutokuwa na hadhi ya kuchezewa mechi za Ligi Kuu.

Lakini kufungiwa au kutokuwa katika ubora unaotakiwa, timu hupelekea kuhamahama viwanja jambo ambalo hupoteza maana ya faida ya kucheza nyumbani na kulazimika kuhamia kwenye mkoa ambao hauna timu ya Ligi Kuu kwa wakati huo.

Viongozi wa timu mtanakiwa kuhakikisha mnatengeneza viwanja ambavyo vitakuwa rafiki kwa wachezaji wengi kucheza na hatimaye kupata matokeo chanya na kuacha tabia ya kuhamahama ambayo imeonekana katika miaka ya hivi karibuni ambapo baadhi ya timu zimetumia zaidi ya viwanja vitatu ndani ya msimu mmoja.


Pia maandalizi hayo yanazihusu timu zitakazoshiriki Ligi ya Championship, hii itawasaidia kuwapa heshima wanachama na mashabiki wenu kujipanga vizuri na kujitokeza kwa wingi katika kila mechi wanayocheza badala ya kuwashtukiza kulingana na aina ya mpinzani unayekutana naye.

Kama timu zinazoitwa ndogo huko Ulaya zimekuwa zikiweka miundo mbinu mizuri, basi si vibaya na timu za hapa nyumbani zikawa na utaratibu huo wa kuboresha viwanja vyake na kuacha kubagua 'kukopi' baadhi ya mambo mazuri kutoka kwa klabu hizo zilizoko kwenye mataifa yaliyoendelea.

Lakini pia umefika wakati TFF na Kamati ya Leseni kuacha kutoa leseni kwa viwanja ambavyo havina sifa ya kutumika katika Ligi Kuu au Ligi ya Championship, ambazo hurushwa mubashara, kwa sababu ya kuendelea kuzipa heshima na hadhi zake ligi hizo.

Kwa hatua ambayo Ligi Kuu Tanzania Bara imefikia, si busara TFF kutoa leseni kwa viwanja ambavyo havina ubora na kufanya hivyo ni kuruhusu 'siasa' za nje kutawala katika soka letu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Tiba vitendo vya ushirikina Ligi Kuu timu zikatwe pointi

**INAONEKANA** kabisa bado imani za kishirikina zinaendelea kutawala katika Ligi Kuu Tanzania Bara, huku kukiwa hakuna hatua madhubuti za kuhakikisha vitendo hivyo vinatoweka.

Adhabu zinaendelea kutolewa na wasimamizi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini badala ya vitendo hivyo kupungua, imani hizo zinaendelea kulitafuna soka la Bongo, kutokana na idadi kubwa ya matukio ambayo yanaonekana kuongezeka kila kukicha.

Kwa mujibu wa taarifa za matukio zilizotolewa hivi karibuni na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi, zinatakiwa juhudi za makusudi zifanyike kuondoa tabia hizi potofu zinazoshangaza katika mechi za Ligi Kuu ambayo huonekana mubashara.

Inashangaza kuona katika karne hii ya 21, bado klabu haziamini wachezaji bora, benchi la ufundi zuri na uongozi bora ili kupata matokeo chanya.

Katika kikao chake cha Aprili 30, mwaka huu, wasimamizi hao walisema Simba na Yanga, hazikutumia milango iliyo rasmi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa katika mechi yao iliyochezwa Aprili 20, mwaka huu, Yanga ikishinda mabao 2-1.

Licha ya kufanya hivyo, timu hizo zote hazikutumia mlango rasmi wa kuingilia vyumbani, huku Yanga ikikataa kuingia katika chumba maalum cha kuvalia, badala yake kutumia eneo la wazi kwa ajili ya maandalizi ya mchezo.

Simba nayo ilitumia chumba maalum kabla ya mchezo, lakini hawakurejea tena wakati wa mapumziko.

Pamoja na mambo mengine, hii imetajwa ni moja ya vitendo vinavyoashiria imani za kishirikina.

Kutokana na hilo, Simba imetozwa faini ya Sh. milioni moja, lakini Yanga ikipigwa faini ya Sh. milioni tano kwa kile kilichoelezwa na kutenda kosa hilo zaidi ya mara moja.

Taarifa inasema Yanga imekuwa ikifanya hivyo tangu msimu wa 2021/22, 2022/23 na msimu huu.

Ukiziacha timu hizo, Mashujaa FC ilifanya vitendo kama hivyo, ambapo wachezaji na viongozi wake walimwaga vitu vyenye asili ya unga kwenye viti vya mabenchi ya ufundi, pamoja na kuweka chupa yenye kimiminika, ikiyokuwa na karatasi nyeupe ndani yake, hivyo kuonyesha ishara ya imani za kishirikina katika mechi yao dhidi ya Azam FC iliyoisha suluhu, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na kutakiwa kulipa faini ya Sh. milioni moja.

Viongozi wa Prisons wanadaiwa kukataa kuingia vyumbani katika mechi yao dhidi ya Geita Gold ikiwa ugenini, wakidai chumba chao kiliwekwa vitu vinavyoashiria imani za kishirikina, lakini walishindwa kuthibitisha. Klabu hiyo pia imetozwa faini ya Sh. 500,000.

Wachezaji wawili wa Coastal Union, Bakari Selemani na Abdallah Denis, pamoja na mchezaji wa Namungo, James Mwashinga, wamepewa onyo kali kwa kosa la kutoingia katika vyumba vya kuvalia wakati wa mapumziko, timu zao zilipokutana kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, Lindi ambapo Namungo ikishinda bao 1-0, jambo ambalo ni kinyume cha kanuni, ambapo nalo linahusishwa na imani za kishirikina.

Pamoja na TFF na Bodi ya Ligi imekuwa ikitumia hili kama vita vya kunguru ni fursa ya panzi kwa kukusanya fedha kutokana na makosa hayo, lakini inashusha hadhi ya Ligi ya Tanzania ambayo imejengwa na vyombo hivi.

Nadhani TFF na Bodi ya Ligi waende mbali zaidi kwa kuzipoka pointi timu zinazofanya makosa hayo.

Mbali na faini, angalau kila kosa la aina hiyo timu ikatwe pointi moja, ili klabu ziumie moja kwa moja wao na mashabiki wao, tofauti na sasa ambapo mashabiki hawaumizwi na adhabu hizo, lakini hata viongozi haziwaumizi kwa sababu faini hizo hawatoi mfukoni.

Endapo adhabu itakuwa kulipa faini pamoja na kupokwa pointi moja, huenda vitendo hivyo vikapungua au vikamalizika.

Mashabiki watakapokuwa wanaumia kwa timu zao kukatwa pointi na kulalamikia uzembe wa viongozi wao, ndipo nao watakuwa makini.



Mchuuzi wa samaki wa kukaanga, Aisha Hassan (kushoto), akimhudumia mteja wake, katika soko la Samaki la Kimataifa la Magogoni, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Kipande kimoja cha samaki kiliuzwa kuanzia bei ya 3,000/-.
**PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Shahidi aeleza wanandoa walivyomjeruhi jirani yao

**Na Grace Gurisha**

MSIMAMIZI wa Msikiti wa Wahindi Lohana, Ankit Dawda (32) ameieleza Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam jinsi wanandoa Bharat Nathwan (57) na Sangita Bharat (54) walivyomshambulia jirani yao, Lalit Ratilal na kutoa matusi ya nguoni kwa lugha ya Kihindi.

Wanandoa hao ambao ni raia wa Tanzania wenye asili ya kiasia, wanaoishi Mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana, Dar es Salaam, wanashtakiwa kwa mashtaka manne likiwamo la kujeruhi, waliyoyatenda Julai 21, 2023 kinyume cha sheria.

Dawda alidai hayo jana mbele Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkuu, Aaron Lyamuya, wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa mashtaka.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, akisaidiana na Frank Rimoy, Dawda alidai kuwa kazi yake ni kusafisha mazingira ya msikiti, kupamba na kutoa mapambo pia kukusanya vitu vya msikiti na kusimamia usafi na ukarabati jengo zima lenye nyumba za makazi na kwamba msikiti huo uko katika jengo hilo.

Alidai kuwa Julai 21, 2023 alikuwa ofisini kwake akiendelea na majukumu yake, ghafla alifuatwa na watu ambao hakuwafahamu wakimweleza kwamba aende akaangalie juu ya ghorofa kuna kelele.

Alidai kuwa alipofika juu, alikuta Sangita Bharat akilalamika na kuwafokea mafundi waliokuwa wakifanya ujenzi katika eneo hilo watoe viroba vya vigae vilivyokuwa katika kibaraza wakati vitu vyote vilikuwa katika eneo la Lalit Ratilal na hakuna kitu kilichopo katika eneo la Sangita Bharat.

Dawda alidai kuwa kwa wakati huo kulikuwa na kelele nyingi, ndipo Sangita Bharat akaendelea kupaza sauti yake kwamba uchafu uliokuwa katika kibaraza chao utoke.

"Kwa sababu mafundi hawakutoa hivyo vigae, Sangita Bharat akaanza kurusha matusi kwa lugha ya kihindi na hapo hapo waume zao wakawasili na Sangita akawa anaendelea kutoa matusi na Kiran Lalit akapigwa na Bharat Nathwani - mume wa Sangita, hadi kuzamisha kichwa chake kwenye ndoo ya saruji akatumbukia huko na mume wake naye akapigwa kifuani, kichwani na mguuni akadondoka chini akazimia.

"Waliita 'ambulance' (gari la wagonjwa) wakamshusha chini wakapelekwa hospitali lakini sikujua ni hospitali gani wamepelekwa,"alidai Dawda

Kesi iliahirishwa hadi Juni 3,2024 kwa ajili ya kuendelea kwa mashahidi wa upande wa mashitaka.

Awali, fundi seremala, Dominic Mpakani (43), aliieleza mahakama mshtakiwa Bharat Nathwan allivyomshambulia jirani wake, Lalit Ratilal, kwa kumpiga kichwa kifuani kisha akadondoka chini na nakupoteza fahamu kwa muda.

Alidai kuwa kulikuwa na ugomvi kati ya mke wa Bharat (Sangita Bharat) na mke wa Lalit (Kiran) ambao walikuwa wakirushiana maneno kwa ukali kwa lugha ya kihindi na baada ya muda kidogo waume zao walifika kwa pamoja na kuingilia ugomvi huo.

Alidai kuwa Julai 21, 2023 alikuwa nyumbani kwa Lalit Ratilal, mtaa wa Mrima katika jengo la Lohana, alimwita kwa ajili ya kumfanyia kazi zinazohusiana na mbao na kazi zingine ndogo ndogo. Alidai kuwa alifika katika jengo hilo saa tatu asubuhi ambapo bosi wake huyo anakaa floor ya tatu, wakati anaendelea na kazi alidai kuwa Sangita alikuwa amesimama kwenye dirisha lake na Kiran alikuwa amesimama kwenye mlango wake, kila mmoja alianza kuzungumza kwa ukali na kwa jazba wakitumia lugha ya kihindi.

"Lakini nilimsikia mke wa Bharat, Sangita akimwambia mke wa Lalit kwamba uchafu wake apeleke huko ambapo vitu vyote vilikuwa vimewekwa katika eneo la Lalit na hakuna kitu chochote kilichokuwa katika eneo la Sangita. Baada ya dakika kadhaa sijui walipiga simu au vipi waume zao walikuja kwa wakati mmoja na malumbano yakaendelea kwa wote wanne," alidai Fundi Mpakani

Shahidi huyo alidai kuwa, wakati malumbano hayo yanaendelea wote walikuwa wamesimama kwenye mlango wa Lalit, baada ya muda Bharat akampiga kichwa Lalit na Lalit akadondoka chini na kupoteza fahamu.

Shahidi mwingine ambae ni Dk Lucia Augustino (52) wa Hospitali ya Mnanzi Mmoja alidai kuwa Julai 21,2023 alikuwa Idara ya Dharura chumba namba 20 muda wa mchana alipokea wateja wawili wenye asili ya kiasia walikuwa wamechafuka kuanzia kichwani hadi miguuni , mama alichafuka sana kuliko baba.

Kwa mujibu wa hati ya mashitaka, washitakiwa hao ambao ni raia wa Tanzania kabila ya kihindi wanaoishi Mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana Dar es Salaam wanatuhumiwa kwa mashitaka manne waliyoyatenda Julai 21,2023.

# Mabadiliko ya tabianchi yachochea ongezeko la vifo vya malaria

**Na Joyce Lameck**

KUTOKANA na lengo la kutokomeza malaria ifikapo mwaka 2030, serikali imesema wagonjwa na vifo vitakanavyo na maradhi hayo vimeongezeka nchini kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, alibainisha hayo jana mkoani Dar es Salaam alipowasilisha salamu za serikali kwenye Jukwaa la Malaria 2024 lililoandaliwa na Taasisi ya Afya Ifakara (IHI).

Prof. Nagu alisema licha ya jitihada zinazoendelea kufanywa na serikali na wadau mbalimbali kutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030, ambao ni ukomo wa upimaji wa Malengo ya Milenia, bado kuna ongezeko la wagonjwa kwa asilimia moja. Pia alisema vifo vitokanavyo na ugojwa huo nchini, vimeongezeka kwa uwiano wa 0.6 kwa kila watu 100,000.

Alisema ongezeko hilo limetokana na mabadiliko ya tabianchi, hususani mvua kubwa iliyonyesha mwaka jana na kusababisha mbu wanaosababisha malaria kuzaliana kwa wingi.

Takwimu zinaonyesha vifo vitokanavyo na malaria Tanzania Bara mwaka 2022 vilikuwa kwa uwiano wa 2.6 kwa kila watu 100,000, lakini vilifikia uwiano wa 3.2 kwa kila watu 100,000 mwaka uliofuata (2023) katika kukabiliana na ugonjwa huo,

Prof. Nagu aliwataka washiriki wa jukwaa hilo kutilia mkazo matumizi ya teknolojia katika kutokomeza malaria nchini.

Alisema wanasayansi wanapaswa kuhakikisha wanatafuta mbinu mbadala za kudhibiti ugonjwa huo licha ya kukabiliwa na changamoto za kifedha; watumie fedha zinazopatikana katika kutokomeza malaria.

"Tunajua kuwa tuna changamoto ya fedha au rasilimali lakini kwa zile zinazopatikana tunatakiwa kuziweka vizuri. Tutoe kipaumbele kwa mambo yenye tija kama vile upuliziaji dawa ambao haujafanyika vizuri katika maeneo unakohitajika," alisema.

Prof. Nagu pia alisema ni muhimu wadau wa jukwaa hilo kutafakari namna jamii yote itakavyofikiwa na huduma za kudhibiti malaria; maofisa afya ngazi ya jamii wawezeshwe kuifikia jamii na kuipa huduma.

Mkurugezi wa IHI, Dk. Honorati Masanja, alisema kutokana na kukua kwa teknolojia nchini, watafiti wanapaswa kutumia njia za teknolojia katika kutokomeza ugonjwa huo.

Alisema tayari wameanza kutumia teknolojia ya akili bandia katika kubambana na ugonjwa huo kwa kukagua matundu yaliyopo kwenye chandarua kama bado kinafaa kwa matumizi au hakiwezi kuendelea kutumika zaidi.

Dk. Masanja alisema utafiti uliyofanywa na taasisi hiyo umegundua chanjo mbili za malaria ambazo ni RTSS na R21, ambazo zimethibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Alisema nchi inapaswa kuzisajili na kufanyiwa tadhimini ili zianze kutumika nchini.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Faustine Ndugulile, aliitaka serikali itekeleze azimio la Bunge la kutumia dawa za kuua wadudu kutoka kiwanda cha ndani cha IHI kilichoko Kibaha, Pwani kutokomeza malaria ya mbu nchini.

Pia alisema serikali inapaswa kutanua wigo wa fedha za ndani kwa ajili ya ununuzi ya viuadudu pamoja na dawa za kutibu malaria.

Vilevile, Dk. Ndugulile ambaye aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Afya, alisema Tanzania inahusika katika utafiti wa chanjo za kuzuia malaria lakini haijanufaiki nazo bali zinanufaisha mataifa mengine ambayo yalishaanza kutumia chanjo hizo.

# Pinda awakumbuka watu wenye ulemavu

**Na Munir Shemweta,** MLELE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amekabidhi baiskeli za wenye ulemavu wa miguu ikiwa ni jitihada za kuwasaidia watu wa kundi hilo.

Pinda ambaye ni Mbunge wa Kavuu mkoani Katavi, alikabidhi baiskali hizo juzi wakati wa mkutano wa hadhara na wananchi wa kijiji cha Kirida katika Kata ya Mamba, Halmashauri ya Mpimbwe wilayani Mlele.

Baiskeli iliyokabidhiwa kwa mwenye ulemavu Adela John, mkazi wa Kirida, ni sehemu ya baiskeli nne zilizotolewa kwa wenye ulemavu wa miguu wa jimbo la Kavuu ili kuwasaidia usafiri wa kuwawezesha kwenda maeneo mbalimbali.

Akizungumza wakati wa kukabidhi baiskeli hiyo, Pinda alisema anatambua adha wanayoipata watu wenye ulemavu wa miguu katika jimbo hilo ndiyo maana ameona kuna haja ya kuwapatia baiskeli zitakazowasaidia kwenda katika shughuli zao. "Ni matumaini yangu kuwa baiskeli hii itakuondolea adha uliyokuwa ukiipata na kwa sasa itakusaidia sana wakati wa kwenda katika shughuli zako,' alisema.

Mapema kwenye mkutano wake na wananchi wa kijiji cha Kirida, Pinda aliwaeleza wananchi kuwa pamoja na kukabiliwa na majukumu ya unaibu waziri, amekuwa akifanya juhudi ya kuwatumikia katika kuwaletea maendeleo.

Alizitaja juhudi hizo kuwa ni pamoja na ujenzi wa barabara, zahanati na vituo vya afya, madaraja na shule za msingi na sekondari sambamba na upatikanaji huduma za umeme na maji.

"Pamoja na kwamba hamnioni mara kwa mara nikija hapa Kirida kutokana na majukumu niliyo nayo, nimekuwa nikifanya kazi kubwa ya kuwaletea maendeleo na haya maendeleo mnayoyaona ni jitihada ambazo ninazifanya," alisema.

Awali, wananchi wa kijiji cha Kirida walimweleza mbunge kuwa wanakabiliwa na changamoto malimbali ikiwamo kutofanyika vikao vya kijiji kwa ajili ya kujua mapato na matumizi, na kuwekewa alama za mipaka maeneo ya nyumba zao kwa madai kuwa makazi hayo yako kwenye kingo ya mto, hivyo kutakiwa kuhama wakati mto ndiyo umehama.

# Sheria usalama barabarani kufanyiwa marekebisho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema ipo katika hatua ya Marekebisho ya kifungu cha nane cha Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 ambacho kinazungumzia usajili wa vyombo vya moto. Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Baraza la Wawakilishi (BLW), Bakar Hamad Bakar.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini vyombo vya usafiri vilivyosajiliwa Zanzibar vitatambuliwa Tanzania Bara.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo, alisema baada ya kupokea maoni ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mapendekezo hayo yatawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zaidi. Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema kwa kuwa mchakato wa marekebisho ya sheria hiyo umechukua muda mrefu, na kuhoji kwanini serikali isione umuhimu wa kuweka mwongozo maalum kipindi hiki wakati yanasubiriwa mabadiliko ya sheria.

Sillo akijibu swali hilo, alisema kwa kuwa serikali ipo kwenye mazungumzo na Zanzibar, Mbunge awe na subira na utaratibu wa sasa uendelee kutumika.




Mhifadhi Mkuu Mwandamizi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Hassan Nguruma (kulia), akipokea cheti cha shukrani kutoka kwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Tanzania Photographers and Videographers (TPVF), Rajab Mchatta, jijini Dar es Salaam juzi, kutokana na udhamini wa shirika hilo katika semina ya mafunzo kwa wapigapicha za mnato na video, hivi karibuni. Kushoto ni Ofisa Habari wa TANAPA, Alais Munka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 19/- zahitajika kuboresha miundombinu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAKALA wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Morogoro inahitaji Sh. bilioni 19 kwa ajili ya kurekebisha miundombinu iliyoharibiwa na mvua na kurejesha hali stahimilivu katika wilaya mbalimbali mkoani hapa.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Ndyamukama, alisema juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa wameshapeleka maombi ya kiasi hicho cha fedha serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Alisema fedha hizo zitatumika katika kuweka mipaka, kufanya usanifu upya, kufanya mabadiliko na kuomba vibali huku wakianza utekelezaji wa kurekebisha miundombinu hiyo.

Hata hivyo, aliishukuru serikali kwa kutoa Sh. bilioni 2.8 baada ya kuanza mvua, hivyo utekelezaji wa kurejesha miundombinu ya barabara utaanza baada ya hali kukaa sawa ndani ya Mei mwaka huu kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

Alisema TARURA kwa sasa inajipanga kukutana na mameneja wote wa wilaya mkoani Morogoro ili kujadili namna ya utekelezaji bajeti yao inayokaribia ukingoni kutokana na uharibifu uliotokea.

"Tulikuwa na mkataba uliokwishatiwa saini kwa ajili ya kazi maalum lakini uharibifu umetokea, kwa hiyo tutajadiliana zaidi kuangalia namna ya kuitekeleza ili tuwe na miundombinu stahimilivu, tusitengeneze kupoteza fedha, huku tukihakikisha fedha zilizotolewa zinafanya matengenezo ya uharibifu uliotokea na wakati huo huo tukisubira maombi ya Sh. bilioni 19," alisema. Mhandisi Ndyamukama alisema mkoa wa Morogoro ni wa kimkakati kutokana na kuzalisha mazao ya kilimo na biashara na kwamba kurejesha huduma za kijamii zikiwamo hospitali, shule na masoko kutasaidia kuendeleza kukuza maendeleo ya mkoa hasa katika Wilaya za Ulanga, Kilombero na Malinyi.

Alisema mvua inayoendelea kunyesha imeharibu takriban sehemu kubwa ya miundombinu kwenye mkoa mzima, hivyo kuvuruga utaratibu wa kawaida wa matengenezo ya barabara waliojiwekea.

Aidha, Mhandisi Ndyamukama alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24 mkoa wa Morogoro ulitengewa Sh. bilioni 26 kwa ajili ya kutekeleza maboresho ya barabara kutoka serikalini kupitia fedha za barabara, mfuko wa jimbo na mfuko wa tozo.

Alisema wakiwa karibu asilimia 50 ya utekelezaji wa mpango wa kawaida wa maboresho ya barabara, mkoa ulikumbwa na mvua ya El Nino na kusababisha utekelezaji wa bajeti husika kusimama.

Awali, akizungumzia athari za El Nino mkoani Morogoro, Mbunge wa Ulanga, Salim Hasham, alitupa lawama kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na TARURA kwa kushindwa kuimarisha miundombinu, hivyo kufanya wilaya hiyo kutofikika kirahisi kama ilivyokuwa awali kutokana na barabara na madaraja kutishia kuvunjika.

# Mbunge aipa ushauri serikali zao korosho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, ameishauri serikali mambo matano kwenye zao la korosho ikiwamo kufuta tozo zinazomuumiza mkulima sokoni.

Akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2024/25 bungeni jana, Chikota alisema mkutano wa tathmini ya zao hilo wa mwaka jana walikubaliana iundwe timu ya wataalamu ya kuangalia mnyororo wa thamani wa korosho ili kubaini kero na kutoa mapendekezo kwa Wizara ili kutafuta ufumbuzi.

"Nimpongeze Waziri aliunda timu ya watu makini na imekuja na ripoti ambayo Wizara imeanza kufanyia kazi niipongeze kwa kazi kubwa iliyofanya ya kuchambua kuanzia uzalishaji, uvunaji na uongezaji thamani,"alisema.

Alisema katika mfumo wa uuzaji korosho timu hiyo ilibaini kuna changamoto na malalamiko na kupendekeza msimu huu uwapo mfumo wa Soko la Bidhaa Nchini (TMX) ambao Serikali imekuja na maamuzi kwa mwaka ujao.

"Wakulima wa korosho wamefurahi uamuzi huu wanachotaka ni bei nzuri ya korosho sokoni na wanufaike na kilimo chao. Nashauri wakati TMX inaingia iangalie changamoto zilizojitokeza wakati tunatumia kwenye zao la ufuta, changamoto ya kwanza wakati ule ilikuwa wahusika kutokuwa karibu na wakulima kitu ambacho tunatarajia msimu huu TMX watakuwa na utaratibu wa kuweka Ofisi jirani na wakulima ili kutatua changamoto zinazojitokeza,"alisema.

Alisema timu hiyo ilibaini tozo nyingi kwenye korosho zinazomuumiza mkulima sokoni na kuomba kama serikali itarudisha mapato ya ushuru wa korosho (export levy) kwa asilimia 50 na kutoa asilimia 100 kwa zao hilo ni wakati sasa wa kuondoa tozo zingine ili mkulima apate bei nzuri sokoni.

"Kwa mapendekezo yangu tozo ambazo tunaweza kuanza nazo ni zile tunazopeleka kwenye Taasisi zinazopata fedha kwa utaratibu mwingine, kwa mfano tozo ya TARI tumeona wanachukua kwenye pamba Sh.Bilioni mbili, nashauri ni vyema kwenye korosho nasi tukatenga fedha na sio kuwakata wakulima kwa kila kilo Sh.25 ukipiga hesabu kila mwaka zinatolewa zaidi ya Sh. bilioni sita kwenda TARI."

Alitaja tozo nyingine ni inayopelekwa Bodi ya Korosho na kwamba ni taasisi ya umma inayoweza kujiendesha kwa ruzuku za kawaida ya serikali kama ilivyo kwa nyingine na hakuna sababu mkulima kuchangia Sh.25 kwa kilo kwa ajili ya uendeshaji wa bodi hiyo na kushauri pia tozo hiyo iondolewe.

"Soko la awali limekuwa chanzo cha vurugu ni muda muafaka kama ilivyopendekezwa na timu wawezeshwe wabanguaji wa ndani, naomba katika soko la awali utolewe mwongozo mpya kuhakikisha halivurugi minanda wakati wa msimu,"alisema

Aidha, alisema timu hiyo iliangalia suala la uongezaji thamani katika kongani ya ubanguaji korosho ya Malanje na kwamba ni wakati wa serikali kujikita kwenye korosho karanga na si kupeleka korosho ghafi nje na itasaidia kupata bei nzuri kwa mkulima wa korosho.

"Wizara imeshapeleka zaidi ya sh.bilioni tano kwa Bodi kukamilisha mradi huu naomba iongeze kasi ya utekelezaji ili kongani ianze kufanya kazi, na kwenye maeneo ambayo bodi imetwaa ardhi wananchi walipwe fidia zao kwa wakati na ujenzi uanze,"alisema.

# Madiwani walia na tembo wavamizi

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Itigi mkoani Singida, limeiomba serikali kuwahamisha tembo ambao wako karibu na makazi ya watu kabla ujenzi wa tuta la mradi wa reli ya kisasa (SGR) haujakamilika ili iwe rahisi kuwarejesha kwenye Hifadhi ya Rungwa.

Wakitoa ombi hilo juzi kwenye kikao cha baraza hilo, walisema tembo wamekuwa kero kubwa hususani katika kata za Mgandu, Sanjaranda na Kitaraja na wanaharibu mazao mashambani na kusababisha vifo vya watu mara kwa mara.

Diwani wa Mgandu, Richard Kapona, alisema tuta hilo litakapojengwa kabla ya kuwahamisha tembo hao kwenye makazi ya watu kutakuwa na uzio hivyo hakutakuwa na mapito hali itakayoleta ugumu kuwahamisha.

Naye Ofisa Mhifadhi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama Tanzania (TAWA) Kanda ya Kati, Winnie Kweka, alisema mamlaka hiyo imekuwa ikichukua hatua ya kuwahamisha tembo hao kutoka kwenye makazi ya watu kwa kutumia mabomu ya pilipili.

Alisema mabomu hayo yanatengenezwa kwa kutumia mchanga ambao unachanganywa na pilipili iliyosagwa na kuwekwa kwenye mpira na kilipuzi ambacho kinakuwa na utambi ambalo hurushwa walipo tembo hao na kulipuka.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itigi, Hussein Simba, alisema serikali imeendelea kuchukua hatua kadhaa za kuwaondoa tembo kutoka kwenye makazi ya watu na kuwasaidia wale wanaopata tatizo la mazao yao kuharibiwa ba tembo hao. Mwaka juzi, Taasisi ya Utafiti wa Wanyama Tanzania (TAWIRI) ilitoa elimu na mafunzo ya utatuzi wa migongano baina ya wanyapori na binadamu kwa kutumia mbinu rafiki za kudhibiti wanyama waharibifu kwa wananchi wa halmashauri ya Itigi.


Taasisi hiyo ilitoa mafunzo hayo kwa wakulima 30 kutoka kata za Mwamagembe, Sanjaranda, Itigi, Majengo na Kitaraka.

Timu hiyo ya wataalamu kutoka TAWIRI iliongozwa na Dk. Janemary Ntalwila, na iliwafundisha wananchi baadhi ya mbinu za kuwadhibiti tembo ikiwa ni pamoja na vitisho vya mwanga,vitisho vya sauti (vuvuzela au honi kali),mabomu ya pilipili, matumizi ya fataki,uzio wa vitambaa vyenye mafuta ya oili na pilipili,Tofali la pilipili na matumizi ya fensi ya mizinga ya nyuki.

Aidha, walifundishwa njia mbadala ya upandaji wa mazao kinga katika maeneo yanayoathirika na tembo kuwa ni njia nzuri ya kupunguza migongano .

Baadhi ya mazao hayo ni pamoja na tumbaku, pilipili, ufuta na tangawizi ambayo yanaweza kupandwa kuzunguka shamba au kama mazao mbadala.

Njia hizo zimethibitika katika maeneo mengi kuwa na matokeo chanya ya kupunguza uvamizi na uharibifu wa mazao na madhara mengine yanayotokana na uvamizi wa wanyamapori hao waharibifu.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akipokea Kitabu cha Safari ya Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka kwa Balozi wa Tanzania nchini Italia, ambaye ni mmoja wa waandaaji wa kitabu hicho, Mahmoud Thabit Kombo, ofisini kwake, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Askofu aonya unyanyapaa kwa wenye ulemavu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASKOFU Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Amon Kinyunyu, ameiasa jamii kutowanyanyapaa watu wenye ulemavu bali wawasaidie ili kutimiza ndoto zao. Akizungumza kwenye uzinduzi wa mradi jumuishi wa kuwasaidia watu wenye ulemavu, Askofu huyo alisema hali hiyo itawaondoa kwenye utegemezi.

Alisema watendaji watakaokwenda kutekeleza mradi huo wahakikishe wanafanya kazi kwa weledi ili kuleta matokeo chanya.

"Naomba watumishi ambao ni wasimamizi, mkafanye kazi kwa bidi ili kuhakikisha fedha zilizotolewa kuendesha mradi huo zinatumika ipasavyo," alisema Kinyunyu.

Naye Askofu wa Dayosisi hiyo, Christian Ndossa, alisema mradi huo utabadilisha maisha ya watu wenye ulemavu na kuwafanya wajisikie kama watu wengine.

Alisema viongozi wa dini wanapaswa pia kujifunza namna ya ufundishaji watu wenye ulemavu ili kuwapa huduma za kikanisa bila kikwazo. Alisema watumishi wakijua lugha za alama itakuwa vyema kwao,kutoa huduma kwa watu wa aina zote pindi wanapokuwa madhabahuni.

"Tunao watu wa aina hii katika nyumba zetu za ibada,tunapaswa kujua lugha za alama,ili tuwasaidie kupata neno la Mungu," alisema.

Naibu Katibu wa Dayosisi na msimamizi wa miradi, Bartholomeo Myanga, alisema mradi huo jumuishi utaleta matokeo chanya kwa watu wenye ulemavu kutokana na usimamizi mzuri utakaofanywa.

Alisema wameamua kufanya hivyo na wamejipanga kuhakikisha unawafikia walengwa wote katika maeno mbalimbali ya kikanisa.





# Waziri ataka ufuatiliaji wabunifu, kuendelezwa

**Na Hawa Abdallah**

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohmed, amesema ni vyema wabunifu ambao wanajikita kubuni mambo mbalimbali katika masuala ya teknolojia kufuatiliwa na kuendelezwa badala ya kuachwa na vipaji vyao kupotea.

Aliyasema hayo wakati akifunga Mafunzo ya Mashindano ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa wanafunzi wasichana 31 kutoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar, yaliyofanyika visiwani hapa juzi.

Alisema wanafunzi hao ambao walikuwa katika mafunzo ya ubunifu kupitia mifumo ya kisasa na hata wengine waliopo nje ya Mafunzo haya lakini wanajulikana kwa ubunifu wao ni vyema kufatiliwa ili kupewa fursa mbalimbali za ajira katika sekta za serikali na hata binafsi pale zinapohitaji watu wa fani hizo.

Alisema ni muhimu ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Technolojia (COSTECH) kuwa na data maalum ya wabunifu wote ambao wamejikita kubuni katika maswala ya mfumo ya tehama ili kuwafatilia na kuangalia namna gani ya kuwasaidia kupitia fursa zinazojitokeza badala ya kuwaacha na kushindwa kuendelea na ubunifu wao.

Alisema anaamini Tanzania na Zanzibar kuna wabunifu wengi lakini kutokana na kutokuwa na mwendelezo kwa wabunifu hao, kunasababisha kushindwa kuendelea na jambo hilo na kujikita katika mambo mengine.

"Leo tumepata wabunifu 31 ambao ni wadogo kabisa kwa maana ni wanafunzi. Je, hawa ambao tunao sasa na wale ambao tumewapa mafunzo kama haya hapo awali tumejua wako wapi? Au hawa ambao tupo nao tumewawekea nini baada ya kumaliza masomo yao au tutaawacha tu bila kuendeleza vipaji vyao hivi vya teknolojia hii?" alohoji.

Pia alisema dunia ya sasa imetawaliwa na matumizi makubwa ya mifumo ya TEHAMA ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo taasisi zilikuwa zikitumia makaratasi katika utunzaji wa taarifa.

Alisema matumizi hayo ya mifumo yawe chachu ya kuleta mafanikio na maendeleo ya haraka katika wakati Tanzania Bara na Zanzibar huku zikiendelea kupiga hatua katika matumizi ya teknolojia ingawa bado haijafika katika hatua kubwa ikilinganishwa na nchi nyingine zilizoendelea.

Pia aliwataka wasichana kutoogopa kusoma masomo ya sayansi kwa kuwa yanasababisha kuwa na uwezo mkubwa wa kufikiria na kutanuka kikali katika kipindi hiki ambacho Serikali zote mbili zipo katika mageuzi ya matumizi ya mifumo ya kidigitali.

Akitoa taarifa ya mafunzo hayo, Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, alisema yalihusisha wasichana 248 katika shule 147 za sekondari ambao walichaguliwa kushiriki kwa kuzingatia ufaulu wa alama za juu katika mitihani ya taifa ya kidato cha pili katika masomo ya sayansi.

# Mvua ya masika yaharibu nyumba 40

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NYUMBA 40 zimeathirika na mvua ya masika inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Kaskazini B, Unguja.

Wakizungumza mbele ya Mkuu wa Wilaya, Hamid Seif Said, hiyo wakati wa ziara ya kuwafariji wananchi walipata maafa na nyumba zao kujaa maji, baadhi ya wakazi hao walisema mvua hiyo imesababisha nyumba kuharibika vibaya nazingine kuporomoka kuta.

Mkazi wa Kilombero, Ali Said, alisema mvua hiyo imeathiri nyumba na kuporomoka kuta na kuanguka, hivyo wamepata hasara ya zaidi ya Sh. milioni tisa kutokana na kuporomoka maeneo makubwa ya nyumba na vitu kuharibika.

Salum Iddi, mkazi wa Kwa Gube, alisema mvua hiyo imeharibu makazi yao na kusababisha hasara kubwa kwa kukosa vitu vya matumizi ya nyumbani na chakula.

"Baada ya kunyesha mvua kubwa, vitu vyetu na vyakula vimeloa na kukokotwa na maji, hivyo kukosa huduma muhimu za makazi na malazi," alisema.

Naye Khadija Saleh, mkazi wa Bumbwini, aliiomba serikali kuwajengea makazi ya kudumu kutokana na nyumba zao kujaa maji na kusababisha mafuriko hatimaye kukosa sehemu za kuishi.

"Hatukutarajia kama mvua itakuwa kubwa kiasi hichi na kukosa makazi. Tunaiomba serikali na wahisani mbalimbali kutupatia makazi kwani hatuwezi kumudu gharama za makazi kwani hali zetu ni duni", alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B, Hamid Seif Said, aliwataka wananchi walipata maafa kuwa na subira kwa kuwa serikali inatambua maafa yaliyojitokeza katika maeneo hayo.

Pia aliwataka wananchi ambao bado wanaishi katika maeneo ya njia za kupita maji, kuhama na kwenda sehemu salama ili kuepuka maafa. "Niwaombe wananchi wetu kusikiliza utabiri wa hali ya hewa na kuacha kukaa sehemu hatarishi ili kunusuru maisha yetu", alisema.

Sambamba na hayo, aliwataka waathirika wa hao kuchemsha maji katika kipindi hiki cha mvua za masika na kuacha kutumia maji ya mashimo kuepuka maradhi ya mlipuko.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma (kulia), Naibu Waziri Anna Athanas na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Khatib Mwadin Khatib (kushoto) wakiteta jambo katika kikao cha kupitia rasimu ya bajeti ya wizara hiyo na Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajawazito wahimizwa kuhudhuria kliniki

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wametakiwa kushirikiana na Wizara ya Afya katika kuwahimiza wajawazito kuhudhuria kliniki mapema ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza katika kikao kazi kwa wataalamu na wadau mbalimbali visiwani Zanzibar. Alisema,vifo vingi vya mama na mtoto vinatokana na baadhi ya kinamama kutohudhuria kliniki na hospitali kwa wakati na mara nyingi hufika hospitalini wakati wa kujifungua hali inayosababisha matatizo ikiwemo kifo.

Katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, alisema Wizara ya Afya imeandaa mikakati madhubuti ambayo ni pamoja na kuwatumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii, wajawazito kuhudhuria kliniki mapema ambapo kwa wahudumu hao watapatiwa mafunzo maalumu mwezi ujao.

Alisema kuna sababu nyingi kwa wajawazito zinazofanya kutopata huduma sahihi ambazo ni pamoja upungufu wa wafanyakazi, vifaa, hata hivyo, serikali kupitia Wizara ya Afya inahakikisha kuwa matatizo yote hayo yanaondoka na mjamzito anapata huduma zilizobora.

Mwenyekiti wa kikosi kazi cha M-mama Zanzibar, Mohamed Habib, alisema mpango huo una lengo la kuhakikisha vifo vya mama na mtoto vinapungua iwapo utatumika vizuri.

Alisema M-mama imekuja kusaidia kuharakisha mjamzito anawahishwa hospitalini na inarahisha kwa wahudumu wa afya kufanya maandalizi na mjamzito kujifungua kwa wakati na kuondokana na matatizo.

Disemba 2022, Zanzibar ilianza rasmi kutumia mpango wa M-mama na hadi kufikia mwaka huu, zaidi ya mama na watoto 2000 walisafirishwa kupitia mpango huo.



**OMONDI**
UKURASA 13

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
JUMAMOSI MEI 4, 2024




# SIKILIZA MIDUNDO
## Nani mkali zaidi?

KUMEIBUKA mjadala mkali katika tasnia ya burudani nchini, baada ya watayarishaji wawili maarufu kuingia katika bifu kwa kila mmoja kujigamba kuwa yeye ndio mkali wa kutengeneza midundo.

Watayarishaji hao, S2Kizzy na Abbah Process wamewagawa wapenzi wa muziki wa Bongo Fleva baada ya kila mmoja kuandika kwenye kurasa zao kuwa ni kinara katika kazi hiyo kuliko mwingine.

Aliyeanzisha sakata hilo alikuwa ni S2kizzy, ambaye aliandika kwenye Insta-Story yake kwamba hataki kufananishwa na mtayarishaji yoyote wa muziki Afrika Mashariki.

Katika ujumbe wake huo amejigamba kuwa yeye ni mtayarishaji bora wa kizazi chake na kwa muda wote.

Hata hivyo, Abbah Process amejibu kwa kuandika kuwa kwa muda wa mwaka mmoja hajakaa studio kuandaa ngoma mpya, lakini bado jina lake linatajwa na kuwa maarufu nchini kote.

"Ni takribani mwaka mmoja sijakaa Studio kutengeneza mdundo ila mitaa inaimba jina langu, wakinyamaza nitaleta mdundo mpya waendelee kujifunza" ameandika Abbah.

Baada ya kuweka jumbe hizo, watu wamevamia kurasa za mitandao ya miamba hiyo ya muziki kwa kutoa maoni mbalimbali kuhusu nani kati yao ni bora kwa kutoa midundo mikali.

BASI SAWA

## Omondi abadili mbinu



MSANII wa uchekeshaji kutoka Kenya, Erick Omondi, amesema ameamua kubadilisha mbinu ya kiuanaharakati baada ya serikali ya nchi hiyo kumuandama kwa kumfungulia kesi lukuki.

Amesema kwa sasa ameamua kuachana na maandamano yake ya kupinga kupanda gharama za maisha, badala yake anakwenda kwa mtu mmoja mmoja kumuinua na kufahamu kinachoendelea.

"Sitaki tena kukamatwa kwa sababu naandamana, nia yangu ni kuwakomboa Wakenya kutokana na serikali kupandisha kila kitu. Ninachofanya sasa namfuata mtu mmoja mmoja kumuinua na yeye atakwenda kwa mwingine hadi mambo yatakuwa sawa," amesema.

## Chameleone kweli msumbufu



MWANAMUZIKI kutoka nchini Uganda, Jose Chameleone, amesema katika suala la mapenzi licha ya kupenda kupita kiasi, lakini ni msumbufu kwa wanawake.

Akizungumza katika sherehe ya kumbukumbu ya siku ya kuzaliwa kwake, Chameleone, amesema ameumbwa akiwa na tabia tofauti za kushangaza ikiwamo mpenda amani, mapenzi na pia ni msumbufu kwa kuwavunja moyo watu wengine.

Mkali huyo wa muziki kutoka lebo ya Leone Island Music Empire, amekuwa akilalamikiwa na mama wa watoto wake watano, Daniella Atim, kuwa ni mnyanyasaji na mtu asiyetabirika akiwa nyumbani.



# HARMONIZE KAWASHA MOTO TENA

MASHABIKI wa msanii maarufu wa Bongo Fleva, Harmonize, kwa mara nyingine wamejikuta wakipigwa butwaa baada ya mkali huyo kutoa maneno yanayoashiria kuachana na muziki.

Sio mara ya kwanza kwa Harmonize kuwachanganya mashabiki wake kutokana na utata wa jumbe zake anazoandika kwenye ukurasa wake wa Instagram, kwani jana aliandika kwamba amechoka na anawaachia wenye muziki wao.

"Licha ya jitihada ninazo ziweka kwenye huu muziki kuhakikisha naweka mchango wangu wa hali na mali ila chuki imekuwa kubwa sanaa, nimechoka nawachia muziki wao" ameandika Harmonize





# Willy Paul alaumiwa kiaina

BAADA ya msanii wa muziki kutoka Kenya, Willy Paul kuachia rasmi albamu yake mpya inayoitwa 'Beyond Gifted', yameibuka malalamiko kuwa umewanyima nafasi wanamuziki wa nchini humo.

Paul amewashangaza mashabiki wa muziki kwa kutomjumuisha msanii yeyote wa Kenya katika ngoma 14 ndani ya albamu hiyo.

Hata hivyo, akijibu tuhuma hiyo Willy Paul amesema aliamua kutowashirikisha wasanii wa Kenya kutokana na tabia zao za kupenda husda na chuki.

FILAMU

# Siri ya Majini: Ukilikoroga utalinywa

**Na Adam Fungamwango**

KUNA msemo wa kiswahili unaosema 'bure aghali'. Maana yake kitu chochote cha bure huwa kina gharama yake. Ukienda mbali zaidi kwenye ufafanuzi ni kwamba chochote kinachoonekana kuwa hakina gharama, huwa kina kasoro, hivyo unaweza kukigharamikia mara kwa mara na kupoteza fedha nyingi, wakati kumbe ungeweza kukinunua kwa gharama kubwa mara noja tu.

Filamu ya 'Siri ya Majini', ina mafundisho mazuri kuhusu hili. Imechezwa na baadhi ya wasanii ambao ni Leah Mussa, Denis Luis, Warda Uwesu, Asha Jumbe, Juma Twalib, Debora Dickson na wengineo.

Ram ana mpenzi wake anaitwa Jacky. Lakini wakati Jacky akiwa safarini Ram anaanzisha mapenzi na msichama mwingine aitwaye Shamim.

Awali ilionekana ni yatakuwa mapenzi ya kawaida tu. Lakini Shamim alinogewa na kumtaka wafunge ndoa awe mkewe. Kutokana na Shamim kuonekana ni msichana mrembo na mwenye uwezo wa kipesa, Ram anakubali.

Hata hivyo, Ram baadaye alikuja kugundua kuwa Shamim hakuwa mke wa kawaida, bali alikuwa jini.

Kujiondoa kwenye mikono ya Shamim haikuwezekana tena, kwani tayari alionekana ameshajua siri hiyo, na Ram alipigwa mkwara wa nguvu kuwa akiondoka kwake, atafayiwa kitu kibaya.

Jacky aliporejea, aliungana na rafiki yake Ram alitwaye Jisu kumsaka na pamoja na kugundua anapoishi, lakini walifukuzwa kama mbwa.

Mapenzi ya biandamu na jini yalifanikisha kuzaliwa mtoto wa kike, lakini akifundishwa tabia zote za kijini na mama yake.

Katika kujiondoa kwenye minyororo ya jini Shamim, Ram anaamua kutafuta mganga ili kumdhuru Shamim, ili arejee nyumbani na kuungana na mpenzi wake aliyempenda kwa dhati, Jacky.

Zoezi linafanikiwa, lakini nusu. Shamim anaungua mwili mzima, na akatambua kuwa zile zote ni njama za mume wake Ram.

Jambo hili linamkasirisha mno jini Shamim. Anamwambia wazi kuwa si jambo la kawaida jini kumlilia au kumpenda binadamu, lakini yeye amefanya hivyo kwa sababu amempenda sana, lakini matokeo yake anakuja kumfanyia mambo kama yale.

Mwisho wa siku, jini Shamim linamuua Ram, lakini jini hilo nalo linauawa, Jacky anabaki peke yake.



# BENDI 5 KALI ZILIZOTIKISA NJE YA DAR

**Na Adam Fungamwango**

KUNA uhaba mkubwa wa bendi za muziki wa dansi kwa sasa. Si mikoani tu, bali hata Dar es Salaam. Kikumbi Mwanza Mpango ambaye kwa sasa ni mgonjwa (Mungu amsaidie), miaka ya 1980 aliwahi kutunga kibao kiitwacho mtoto wa mjini. Hiki pamoja na maudhui mengine, lakini kilizitaja bendi mbalimbali.

Hapa nataka nikutajie tu jinsi gani alivyozitaja kwa kuimba. Lengo ni kukuonyesha ni jinsi gani bendi zilivyokuwa nyingi. Na alizozitaja karibuni zote ni za Dar es Salaam.

"Ukiwakosa wana Kamanyola pitia Sikinde Ngoma ya Ukae. Usisahau Msondo Ngoma, Wana Chakachua pia usubiri. Mwendo wa Jongoo na Super Bomboka huporomosha. Mwenge ya Mashujaa, Kimulimuli huporomosha. Mzee Makassy, Polisi, Kumbakisa huporomosha, Wana Kimbunga na UDA pia huporomosha." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo. Hii inaonyesha kuwa zamani kulikuwa na bendi nyingi sana. Na zote zilikuwa zinapiga muziki mzuri na kuwa na wanamuziki maarufu sana nchini. Lakini pia mikoani kulikuwa na bendi kubwa zilizokuwa maarufu na tishio kwa bendi kubwa za Dar es Salaam.

### Morogoro Jazz Band

Ni moja kati ya bendi maarufu sana nchini Tanzania, Afrika Mashariki na tishio kwa bendi za jijini Dar es Salaam kama Dar Jazz, Western Jazz, Nuta Jazz, na nyinginezo.

Ikumbukwe kuwa bendi hii ndiyo alikuwa akiipigia Mbaraka Mwinshehe.Ilikuwa ni miaka ya 1960, hadi katikati ya miaka ya 1970. Haihitaji maelezo mengi sana kujua umahiri wake. Cha kuongeza ni kwamba mkoani Morogoro kulikuwa pia na bendi nyingi kali kama Cuban Marimba, Kilombero Jazz, Kilosa Jazz, Ulanga Jazz na nyinginezo, ikiwemo aliyoianzishwa mwenyewe Mbaraka mwanzoni mwa miaka ya 70, akaiita Super Volcano.

### Jamhuri Jazz Band

Hii pia ni moja kati ya bendi zilizotingisha nchini Tanzania, Kenya na Uganda. Maskani yake ilikuwa ni Tanga. Hii ndiyo bendi ambayo wametokea wanamuziki waliokwenda kuunda bendi ya Simba Wanyika na kutia fora nchini Kenya, Wilson Peter na mdogo wake, George Peter.

Mbali na bendi hiyo, Tanga kulikuwa na bendi nyingine kali, Atomic Jazz na Amboni Jazz ambazo pia zilifanya vema sana. Hii ilikuwa ni miaka ya 1960, hadi mwishoni mwa 1970.

### Kurugenzi Jazz Band

Mkoani Arusha kulikuwa na bendi iliyoitwa Kurugenzi Jazz. Ni bendi ambayo nayo ilikuja kutetemesha bendi nyingi nchini. Nyimbo kama 'Wivu' na 'Ujamaa Hautakufa', zilipigwa na bendi hii.

Asili ya bendi hii ni wanamuziki wa Morogoro waliojiengua kutoka Morogoro Jazz, Cuban Marimba, na Super Volcano waliokuwa nchini Kenya na kuunda bendi ijulikanayo Orchestra Lombe Lombe.

Baada ya kupokonywa vyombo nchini Kenya kwa kukiuka masharti ya mikataba, Halmashauri ya Arusha iliwapa vyombo na kuwahamisha kutoka nchini humo na kuleta hapo na kuwa Kurugenzi Jazz. Hata wimbo wa 'Wivu' upo ambao uliorekodiwa Kenya, wakati huo ikiwa Lombe Lombe. Ilitamba miaka ya 1970, hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990.

### Tabora Jazz Band

Bila shaka haiitaji maelezo mengi kujua kuwa hii ni bendi maarufu, kubwa na bora kabisa nchini Tanzania ikiwa na maskani yake mjini Tabora miaka ya 1960, hadi mwishoni mwa miaka ya 1970.

Mbali na Kutamba na vibao kama 'Dada Asha', imetoa wanamuziki bora waliokwenda kwenye bendi nyingi kama Shem Karenga aliyekwenda KM Beats 'Tukunyema', Msafiri Haroub aliyekwenda Mwenge jazz.

### Tancut Almasi Orchestra

Ni bendi ya mkoani iliyokuwa na wanamuziki wa Kikongomani wengi kuliko nyingine yoyote ile nchini. Kyanga Songa, Kasaloo Kyanga, Kawele Mutinamwa, Kalala Mbwebwe, Kabaa Belela na wengineo. Ilitamba kwenye miaka ya 1980. Ilikuwa ikija Dar, bendi zote zinakimbia mji na kukimbilia kufanya ziara mikoani kuwakimbia. Makao yao yalikuwa ni Iringa. Walijiita Mabush Stars 'Kinye kinye kisonzo tisa kumi Mangala'.



# Kim, Odell wao kimyakimya

IMEKUWA kama jinamizi baya linazidi kumwandama Kim Kardashian tangu aachane na aliyekuwa mume wake Kanye West, baada ya uhusiano wake mpya na mcheza mpira wa mikono nchini Marekani, Odell Beckham Jr, kuvunjika rasmi.

Watu wa karibu wa wanandoa hao waliliambia jarida la PEOPLE kwamba mapenzi ya wawili hao yamepungua na hatimaye kuisha bila mbwembwe nyingi.

Kim na Odell ambao kwa mara ya kwanza waliibukia kwenye uchumba Septemba 2023, wameamua kutengana kwa amani baada ya kila mmoja kushindwa kuvumilia kinachoendelea kati yao.



## Macaroni huo ni uchoyo

MCHEKESHAJI kutoka Nigeria, Macaroni amekiri kwamba bado hajaoa kutokana na hofu yake ya kugawana chakula cha asubuhi ambacho kwake ni muhimu.

Katika mahojiano na redio moja, Macaroni amesema hatafuti uhusiano wa kimapenzi, ingawa ana mtu ambaye anampenda sana.

Akiwa na tabasamu pana, ameeleza kwamba anakwepa mapenzi kwa sababu hataki kuuvunja moyo wake.

"Maisha yangu ya mapenzi yapo katika hali ya chini, siwezi kuwasemea wanawake ambao wanaweza kuwa wanitazama lakini naweza kujisemea mwenyewe. Nina mtu ambaye ninamkubali," amesema.


## Celine Dion atoa matumaini

MWANAMUZIKI maarufu wa muziki wa Pop, Celine Dion, amewashangaza mashabiki wake baada ya kutokea katika jarida maarufu la Vogue, akisema ana matumaini ya kushinda

katika mahojiano yake na jarida hilo, Dion alieleza kwamba yeye ni mwanamke ambaye anaangalia matumaini ya siku zinazokuja, licha ya kuwa katika mapambano na ugonjwa wa kukakamaa misuli unaomsumbua.

"Nimejivunia kupata nafasi ya kuweka picha yangu kwenye Vogue France nikiwa na umri wa miaka 55. Niliulizwa nini uzuri wangu. Nikashangaa uzuri ni nini? Uzuri ni wewe, ni mimi, ni ndoto zetu, leo mimi ni mwanamke ninayeangalia siku zijazo kwa matumaini,@ amesema katika jarida hilo.





## Rema acha kabisa

MKALI wa Afrobeats kutoka Nigeria, Divine Ikubor maarufu kama Rema, amejiweka katika kundi moja na wanamuziki maarufu Burna Boy, Wizkid na Davido.

Msanii huyo kutoka lebo ya Mavin Records, aliwaambia mashabiki zake kwamba yupo katika orodha ya wasanii wakubwa wanaojulikana duniani.

Amesema kwa sasa hakuna tena kundi la mapacha watatu Burna Boy, Wizkid na Davido ambao wanajulikana katika tasnia ya muziki ya Nigeria bila kutaja jina lake.

## Waliomuua AKA kupewa dhamana?

MAHAKAMA nchini Afrika Kusini inatarajiwa kutoa hukumu kuhusu ombi la dhamana la watu watano ambao wanashtakiwa kwa mauaji ya mwanamuziki Kiernan Forbes maarufu kama AKA na rafiki yake Tebello Motsoane anayejulikana Tibz.

Wawili hao waliuawa kwa kupigwa risasi nje ya mkahawa mmoja mjini Durban mwaka jana.

Washtakiwa watano, Lindokuhle Mkhwanazi, Lindani Ndimande, Siyanda Myeza, Mziwethemba Gwabeni na Lindokuhle Ndimande, walikuwa mahakamani juzi wakati mawakili wao wa utetezi wakihitimisha hoja zao za mwisho katika ombi la dhamana.





# Askari uhifadhi wapigwa msasa biashara haramu wanyamapori

**Na Godfrey Mushi,** LONGIDO

SHIRIKA la World Wildlife Fund (WWF), limeanza kuwapiga msasa askari wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Enduimet (WMA) na Wilaya ya Longido, mkoani Arusha kuhusu namna bora ya kukabiliana na biashara haramu ya wanyamapori na kuheshimu haki za binadamu.

Askari 38 kutoka Enduimet WMA na Jumuiya mpya ya Uhifadhi ya LOKEEN-NATRON, wanajifua kwa wiki nne kuhusu ukamataji salama wa watuhumiwa ili kuwezesha kusaidia kesi mahakamani kuwa na ushahidi wa uhakika usioacha shaka ndani yake.

Meneja Mradi wa WWF, Gasto Mushi, alisema jana kuwa mradi huo unalenga kuiwezesha jamii kujishughulisha na shughuli za uzalishaji mali, kutoa mafunzo ya ulinzi wa wanyamapori, kutoa elimu kwa jamii kupitia klabu za mazingira shuleni na kuboresha ushirikianao na ujirani mwema kati ya Tanzania na Kenya.

"Tunatarajia kupitia mafunzo haya ambayo askari wetu wamepatiwa, yatakuwa chachu ya kuwawezesha kutokomeza biashara haramu ya wanyamapori katika eneo la Enduiment na Wilaya nzima ya Longido, kwani kwa mafunzo haya, matukio yatakuwa yakiripotiwa kabla hayajatokea au uhalifu kufanyika," alisema Mushi.

Mafunzo hayo yanaendeshwa na WWF, kupitia miradi miwili IWT (Illegal Wildlife Trade) na BMZ Unganisha.

Kwa mujibu wa Mushi, miongoni mwa mafunzo waliyopatiwa askari hao ni pamoja na elimu juu ya biashara haramu ya wanyamapori na namna ya kuendesha operesheni mbalimbali.

Imo pia elimu juu ya biashara haramu ya mihadarati, mafunzo ya ukamataji salama wa watuhumiwa ili kuweza kusaidia kesi katika mahakama, elimu ya rushwa, utaratibu wa ukusanyaji wa vidhibiti mbalimbali, elimu ya haki za binadamu, ukusanyaji wa kodi pamoja na udhibiti wa mipaka.

Aidha, Mwenyekiti wa Enduimet WMA, Parsanga Mollel, aliomba wafadhili waliowezesha mafunzo hayo kwa askari, kuyafanya kuwa endelevu huku akiwapongeza askari hao kwa kuhitimu mafunzo yao, akiwataka kuyafanyia kazi ili yawe na manufaa kwa jamii ya Longido na taifa zima.

"Naomba niwajulishe kuwa mafunzo mliyoyapata ni bahati kwani kuna wengine waliyo tamani lakini hawajapata, hivyo niwape hongera na mkayafanyie kazi yote mliyo fundishwa kikubwa mkawe na heshima kwani hakuna kazi bila heshima," alisisitiza Mollel.

Akifunga mafunzo hayo, Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Longido, Mwazani Mohamed, alisema mafunzo hayo yameandaliwa kimkakati ili kuwaongezea ujuzi, nidhamu, ufahamu na uelewa wa namna bora ya kutatua changamoto ambazo zimekuwa zikizunguka eneo la Enduimet WMA.

"Tunatarajia kupata matokeo chanya kutokana na mafunzo kutoka idara mbalimbali waliyo patiwa askari, lakini pia ni muhimu kuwasaidia wananchi kufikia malengo katika uhifadhi na ufugaji na hii itasaidia kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyama," alisema.

# Serikali yapokea ushauri TUCTA

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI imesema imepokea ushauri wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini (TUCTA) la kuiwezesha Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) kuboresha huduma zake.

Juzi, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alieleza nia hiyo ya serikali, alipojibu hoja ya hotuba iliyowasilishwa na TUCTA katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Arusha.

Alisema serikali kwa kutambua umuhimu wa CMA na ushauri wa TUCTA, itaiwezesha kupata vitendea kazi pamoja na kuongeza nguvu kazi ili kuboresha huduma zake ikiwa ni pamoja na kuwapatia magari kwa ajili ya usafiri ili kuwafuata walalamikaji wa migogoro ya kikazi walioko mbali na ofisi za tume.

Katibu Mkuu wa TUCTA, Henry Mkunda, wakati akiwasilisha hotuba yake alisema kuiwezesha tume hiyo kutasaidia kuimarisha ufanisi na wafanyakazi kupata haki zao hasa walioko Katikati ngazi ya Wilaya ambako huduma hazipatikani.

Alisema CMA itasaidia kutatua changamoto ya migogoro ya wafanyakazi katika mikoa na ngazi ya wilaya ambako kumeonekana kukosa huduma hiyo hivyo kuwanyima wananchi haki yao.

CMA ni taasisi huru inayoshughulika na utatuzi wa migogoro ya Kikazi Tanzania bara, baina ya Mwajiri, mwajiriwa pamoja na vyama vya wafanyakazi.

Dira ya CMA ni kuwa na mahusiano mema mahali pa kazi. Wakati dhima kutatua migogoro ya kikazi kwa njia ya usuluhishi na uamuzi katika kukuza ustawi wa jamii na kiuchumi.



Mkuu wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Lazaro Twange (katikati), akisalimiana na Mkurugenzi wa kampuni ya Mati Super Brands Ltd, David Mulokozi alipotembelea banda la kampuni hiyo kwenye maadhimisho ya Sikukuu ya Mei Mosi katika uwanja wa Tanzanite Kwaraa, mapema wiki hii. **PICHA: GIFT THADEY**

# Maofisa waonywa kuinglilia mifumo malipo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, ameonya baadhi ya maofisa utumishi wanaoingia katika mfumo shirikishi wa taarifa za kiutumishi na mishahara (New HCMIS) kusimamisha mishahara na makato ya mishahara ya wenzao bila kufuata taratibu zilizowekwa kwa lengo la kuwakomoa.

Akizungumza jana jijini hapa katika ufunguzi wa mkutano wa 11 wa mwaka wa Jumuiya ya Utawala wa Umma kwa Kanda ya Tanzania, Simbachawene alisema maofisa utumishi wameaminiwa na kupewa dhamana ya kuingia katika mifumo hiyo, hivyo wanapaswa kutumia dhamana waliyopewa kwa uadilifu mkubwa, ili kuondoa malalamiko yanayoonesha uvunjifu wa maadili na ukiukwaji wa taratibu za kiutendaji.

Pia alionya baadhi ya maofisa wenye tabia ya kutoa taarifa ambazo wanakutana nazo katika mifumo hiyo kwa watu wasiohusika.

"Nyie mmeaminiwa vizuri mkabadilika kwa kusimamia maadili na miiko ya kazi zenu, kwa kujiepusha kutoa taarifa za mifumo kwa watu wasio wahusika," alisema. Kwa mujibu wa Simbachawene, ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma; na kuongeza uwajibikaji na uwazi wa watoa huduma na wapokea huduma, kuanzia tarehe 2 Aprili mwaka 2024, ililekezwa uhamisho wa watumishi ushughulikiwe kupitia mfumo wa e-uhamisho. "Ni dhahiri kuwa ushughulikiaji wa uhamisho kupitia mfumo huo, utasaidia kuondokana na changamoto za udanganyifu na upendeleo unaoweza kujitokeza, kutokana na mahusiano kati ya mtoa huduma na mpokea huduma,"alisema.

OR-MUUUB kama msimamizi wa Utawala na Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma, imekuwa ikipokea mrejesho juu ya utendaji wao.

"Baadhi ya maeneo yanayolalamikiwa ni pamoja ucheleweshaji wa upatikanaji wa stahiki za watumishi, kutoa lugha zisizofaa kwa watumishi na wateja, na kushindwa kusimamia maadili ya watumishi ipasavyo,"alisema.

Aidha, alisema waache kushughulikia hoja za watumishi ambazo zinapaswa kumalizwa katika ngazi ya waajiri na badala yake kuacha watumishi kutafuta suluhisho kwa viongozi wa kisera na viongozi wakuu wa kitaifa si sahihi. Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wataalam Tawi la Tanzania (AAPAM Chapter- Tanzania), Leila Mavika, alisema mkutano huo ni sehemu ya kujegeana uzoefu na kaulimbiu yake ni 'Usimamizi wa Utendaji Kazi Katika Utoaji wa Huduma: Nafasi ya TEHAMA Katika Kuimarisha Utendaji Kazi Katika Utumishi wa Umma".

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Buriani Andanenga, nguli fasihi, mtaalam wa mashairi

**Na Adam Fungamwango**

TANZANIA imempoteza, mtaalam wa ushairi na nguli wa lugha ya Kiswahili, Amir Sudi Andanenga aliyefariki usiku wa kuamkia Mei Mosi, kwenye Hospitali ya Dk. Mvungi, jijini Dar es Salaam.

Andanenga, ambaye pia ni mtunzi wa vitabu ambavyo vimewahi kuingia kwenye mitaala ya elimu nchini, alifariki dunia akiwa na miaka 88 na kuzikwa Mei Mosi katika Makaburi ya Kinondoni Shamba, maeneo ambayo alikuwa akiishi mkongwe huyo.

Ni bahati mbaya tu tuko kwenye kizazi cha watu ambao wengi wao ni vijana zaidi ambao hawajawahi kuona kazi zake, au kusikia tunzi, na kusoma mashairi ya Andanenga ambaye mbali na kuwa na tatizo la kutoona, lakini alikuwa na kipaji kikubwa cha kuandika mashairi, vitabu, lakini pia kuwa mahiri wa lugha adhimu ya kiswahili.

Hata baadhi ya watu waliosoma vitabu vyake na kufahamu umahiri wake wanaona mazishi yake hayakuwa na hadhi ya kile ambacho amekitoa kwenye taifa hili kwani hadhi yake ni sawa kabisa na kina hayati, Shaaban Robert, Saadani, Abdul Kandoro, Sheikh Kaluta Amri Abeid, Mathias Mnyampala na wengine wengi.

Kwa wasiomfahamu mzee huyo, alikuwa na kipaji kikubwa cha kutunga mashairi na kwa bahati nzuri amefanya kazi hiyo na watu wa vizazi nyote kuanzia kina Shaaban Robert mpaka hawa wa sasa.

Inasemekana kuwa pamoja na kwamba umahiri wa ushindani wa watunga mashairi ulianza kupungua katikati ya miaka ya 1990, lakini yeye aliendelea kujipambanua kuwa bado alikuwa anaendelea kupambana, huku akiwatungia baadhi ya wasanii wa bongo fleva mashairi yenye mistari na vina ambayo walikuja kuyatumia kwenye nyimbo zao.

Taarifa zinasema kuwa wasanii kibao walikuwa wanakwenda kwake, na kuomba kutengenezewa mistari ya mashairi kutokana na maudhui ambayo wanayahitaji na amekuwa wakifanya hivyo, akitumia muda mfupi kutoana na kipaji alichopewa na Mwenyezi Mungu.

Mwanafasihi huyo alikuwa pia ni mwasisi wa Chama cha Usanifu Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA).

Wakati wa uhai wake alisema, aliwahi kuwa mfanyakazi wa Serikalini katika Ofisi za Bunge, akiwa kama karani, kabla ya kuhamishiwa Idara ya Maji, na mwaka 1972, ndipo maradhi ya macho yalipompata, akafanyiwa operesheni ambayo haikufanikiwa, baadaye macho alipoteza nuru na kutoona kabisa.

Mbali na kupata tatizo hilo, halikuzima kipaji na ndoto zake za kuwa mtu maarufu, badala yake aliendelea kutoa kazi mbalimbali ikiwemo 'Diwani ya Ushadhi', yeye mwenyewe akijipachika jina la 'Sauti ya Kiza' kutokana na hali aliyokuwa nayo.

Baadhi ya vitabu vingi alivyoandika vilitumika kufundishia katika shule za msingi na sekondari, baadhi pia vilitumika katika vyuo vya elimu za juu.



Hayati Amir Sudi Andanenga.

Alizaliwa Oktoba 2, 1932, Kilwa mkoani Lindi na akusoma kaatika shule ya msingi Kikole huko huko Kilwa mwaka 1949, na baada ya hapo alikwenda kusoma elimu ya kati, Songea mkoani Ruvuma, lakini alishindwa kuendelea kutokana na kukosa ada.

Alianza kutambulika rasmi katika uwanda wa mashairi kuanzia mwaka 1954.

Moja ya shairi lake ambalo alilitunga miezi michache tu kabla ya Tanganyika kupata uhuru ni lile alililoiita 'Nyerere awe Rais.'

"Naishika karatasi, na wino wangu nirembe, nirembe jimbo la Kusi, wasomi wa Unyanyembe, Unyanyembe kwa watusi, kunako nyumba za Tembe, Tanganyika aipambe, Nyerere awe rais."

Ni baadhi ya maneno yaliyo kwenye shairi hilo, na kwelie alichokiandika kikatimia. Mwalimu Julius Nyerere akawaongoza wananchi utumwani, akawa Rais wa Kwanza wa Tanganyika huru, ambayo baadaye ikawa Tanzania mwaka 1964 ilipoungana na Zanzibar.

Kama shule moja jijini imepewa jina la mtunzi wa vitabu vya fasihi na mshairi, Shaaban Robert, na Uwanja wa Mpira wa Miguu, jijini Arusha ukapewa jina na mshairi mwingine, wakauita Sheikh Amri Abeid, basi nadhani serikali kwa kuenzi kile alichofanya, haitosita kuipa barabara, shule au uwanja wa mpira jina la Andanenga.

**Tuma meseji 0716 350534**



Baadhi ya marafiki, ndugu, jamaa na watu wa kada mbalimbali, walioshiriki mazishi ya nguli wa kiswahili na mshairi maarufu nchini, Amir Sudi Andanenga..

HABARI KIMATAIFA

# Uturuki yasitisha biashara na Israel

**ISTANBUL,** UTURUKI

SERIKALI ya Uturuki imesitisha shughuli zote za kibiashara na Israel, kupinga mashambulizi yanayoendelea Ukanda wa Gaza.

Hatua hiyo ilielezwa kuwa ni kuonyesha kasiriko lake kutokana na janga la kibinadamu linalozidi kuongezeka katika eneo hilo linalokaliwa na Wapalestina.

Wizara ya biashara ya Uturuki ilisema kuwa hatua hizo zitaendelea kudumu Israel itakaporuhusu mtiririko usioingiliwa wa uingizwaji misaada ndani ya Gaza.

Biashara kati ya nchi hizo mbili ilikuwa na thamani ya karibu dola bilioni 5.6 kwa mwaka jana.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Israel, Israel Katz, alimshutumu Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, kwa kuwa dikteta.

Israel Katz alisema kupitia kwenye mtandao wa X kwamba Rais Erdogan, anapuuza maslahi ya watu wa Uturuki na wafanyabiashara kwa kupuuza makubaliano ya biashara ya kimataifa.

Aliongeza kuwa ameiagiza wizara ya mambo ya nje kutafuta njia mbadala za kufanya biashara na Uturuki, kwa kuzingatia uzalishaji wa ndani na uagizaji kutoka nchi nyingine.

Katika taarifa iliyotolewa na Uturuki ilisema ilisitisha biashara zote.

"Uturuki itatekeleza kwa uthabiti na hatua hizi mpya zitaendelea hadi pale serikali ya Israel itakaporuhusu mtiririko usioingiliwa na wa kutosha wa misaada ya kibinadamu hadi ndani ya Gaza." Ilisema taarifa hiyo.

Mnamo 1949, Uturuki ilikuwa nchi ya kwanza yenye Waislamu wengi kuitambua Israel, lakini uhusiano umezidi kuwa mbaya katika miongo ya hivi karibuni.

Ilipofika 2010, ilivunja uhusiano wa kidiplomasia na Israel baada ya wanaharakati 10 wa Uturuki wanaoiunga mkono Palestina kuuawa katika makabiliano na makomando wa Israel waliopanda meli inayomilikiwa na nchi hiyo kujaribu kuvunja kizuizi cha baharini kilichowekwa na Israel Ukanda wa Gaza.

Uhusiano ulirejeshwa mnamo 2016, lakini nchi zote mbili ziliwafukuza wanadiplomasia wakuu miaka miwili baadaye katika mzozo juu ya mauaji ya Israeli ya Wapalestina huku kukiwa na maandamano kwenye mpaka wa Gaza na Israeli.

Rais Erdogan alizidi kuwa mkali katika ukosoaji wake dhidi ya Israel tangu shambulio lililofanywa na Hamas dhidi ya Israel Oktoba 7, mwaka jana.

Januari mwaka huu, alisema mashambulizi ya kijeshi ambayo Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu sawa na yale aliyofanya Hitler.

Netanyahu alimjibu kuwa hata yeye Erdogan, anafanya mauaji ya halaiki dhidi ya Wakurdi na anashikilia rekodi ya dunia ya kuwafunga wanahabari wanaopinga utawala wake.

**BBC**



Raia wa Rubaya wilayani Musisi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, wakikimbia baada ya waasi wa M23 kuliteka eneo hilo. **PICHA: AFP**

# Marekani yaendelea kuisaidia Burkina Faso

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imeahidi kutoa msaada wa karibu dola milioni 55 kushughulikia mzozo wa kibinadamu nchini Burkina Faso. Akitoa taarifa hiyo, Mkuu Ofisi ya Misaada ya Kiutu ya Marekani, Samantha Power, alisema msaada huo utahusu mahitaji ya dharula.

Alisema msaada huo wa dharura utajumuisha chakula, lishe na mahitaji mengine.

Power alieleza kwamba msaada huo wa fedha utapitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa nchini Burkina Faso, ambao unafikia karibu dola milioni 158, tangu 2023.

Taarifa ya Power ilisema kwamba kuongezeka kwa migogoro na mizozo ya kibinadamu nchini humo kunaonekana wazi kwa jamii zilizotengwa na jicho la huruma la ulimwengu.

Burkina Faso ni mojawapo ya mataifa kadhaa katika Sahel barani Afrika, linalokabiliana na uasi wenye muungano na kundi la Al Qaeda ambalo limesababisha vifo vya maelfu ya watu na wengine kukimbia makazi yao.

Wakati huo huo, Marekani ilisema bado inashirikiana na nchi jirani za Niger na Chad, licha ya kuwaondoa wanajeshi wake katika mataifa hayo.

Ofisa mkuu wa jeshi la Marekani barani Afrika, Jenerali Michael Langley, alisema kwamba makumi ya wanajeshi wa nchi hiyo waliondoka Chad baada ya viongozi wa kijeshi wa nchi hiyo kueleza wasiwasi wao kuhusu kuwepo kwao kabla ya uchaguzi utakaofanyika Mei 6, mwaka huu.

Mwezi uliopita, wanajeshi wa Marekani waliondoka nchi jirani ya Niger baada ya kuagizwa na jeshi la nchi hiyo.

Katika hatua nyingine, wakufunzi wa kijeshi kutoka Russia wamewasili Niger kama sehemu ya makubaliano mapya yaliyofikiwa na viongozi wa kijeshi.

**DW**

# Rais Ruto aagiza shule kutofunguliwa

**NAIROBI,** KENYA

RAIS wa Kenya, William Ruto, ameagiza kuahirishwa ufunguzi wa shule kufuatia nchi hiyo kukumbwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha.

"Naagiza shule ambazo zilikuwa zifunguliwe Jumatatu zisifunguliwe mpaka pale serikali itakapotoa muongozo zaidi" alisema Rais Ruto.

Agizo hilo limetolewa ikiwa zimesalia siku chache kabla ya Mei 6 muda ambao ulikuwa umetangazwa kufunguliwa kwa shule nchini humo.

Awali shule hizo zilipangwa kufunguliwa Aprili 29, lakini iliahirishwa na Waziri wa Elimu, Ezekiel Machogu kutokana na mvua kunyesha.

Machogu alisema wamepata taarifa kuwa baadhi ya shule zimeathiriwa vibaya na mafuriko yanayoendelea.

Alisema kuwapeleka wanafunzi na wafanyikazi katika shule hizo zilizoathiriwa kutakuwa ni kuhatarisha maisha yao.

Awali, wizara ya elimu ilitoa mwongozo kwa kusema kuwa wazazi na wasimamizi wa shule watawajibika kwa usalama wa wanafunzi pale shule zitakapofunguliwa. Pia iliongeza kuwa familia zilizoathiriwa na mafuriko ambazo kwa sasa zinaishi katika taasisi za serikali zitahamishwa katika maeneo mengine.

Katika hotuba yake, Rais Ruto alisema huenda Kenya ikakabiliwa na kimbunga cha kwanza kinachoitwa Hidaya kinaweza kupiga wakati wowote na kuongeza kwamba Idara ya Hali ya Hewa ya Kenya na Kituo cha Utabiri wa Hali ya Hewa cha IGAD, wameshatoa onyo.

"Taarifa za hali ya hewa zinatoa taswira ya kutisha. Mvua zitaendelea kunyesha kwa muda na kasi kwa kipindi kizima cha mwezi huu na pengine baada ya hapo," alisema.

"Kimbunga hicho kinatabiriwa kusababisha mvua kubwa, upepo mkali na mawimbi yenye nguvu na hatari, ambayo yanaweza kutatiza shughuli za baharini katika Bahari ya Hindi na makazi ya watu kwenye pwani ya Kenya." alisema

**BBC**

# Jela maisha kulawiti mtoto wa miaka minne

**Na Hamisi Nasri, Masasi**

FADHILI Shaibu (36), mkazi wa kijiji cha Chiwale, Masasi mkoani Mtwara, amehukumiwa kifungo cha maisha jela baada ya kukutwa na hatia ya kumlawiti mtoto wa kike wa kaka yake mwenye umri wa miaka minne (jina linahifadhiwa).

Shaibu alifanya kitendo hicho baada ya kumshawishi mtoto huyo kwa kumpa machungwa.

Hukumu hiyo ilitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Masasi, Batista Kashusha, baada ya mahakama kujiridhisha na vielelezo vya ushahidi vilivyotolewa mahakamani na upande wa Jamhuri pamoja na upande wa mashtaka.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kashusha alisema kesi hiyo namba 93 ya mwaka 2023 ilikuwa na mashahidi watano na mahakama imemtia hatiani mshtakiwa kwa kumhukumu kifungo cha maisha jela baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa.

Hakimu alisema alisema mshtakiwa alifanya kosa hilo la kumlawiti mtoto wa kike ambaye ni mtoto wa kaka yake Agosti 25, 2023 majira ya saa 9:30 jioni akiwa nyumbani kwake, jambo lililomsababishia maumivu makali na kumharibu sehemu zake za siri.

Alisema mshtakiwa kabla ya kufanya kosa hilo, alifika nyumbani kwa mtoto na kumkuta mama yake ambaye ni shemeji yake akiwa naye ndipo alipomchukua na kuondoka naye kwa madai kuwa anakwenda kumnunulia machungwa kwa kuwa siku zote alikuwa akimwomba amnunulie matunda hayo.

Hakimu Kashusha alisema mshtakiwa alipofika neye nyumbani kwake majira ya saa 9:30 alhasiri, aliingia naye chumbani kwake na kuanza kumlawiti, hivyo kumsababishia madhara makubwa sehemu zake za siri.

Alisema mtoto aliporudi nyumbani, alimwelezea mama yake kitendo alichofanyiwa na mshtakiwa ambaye ni baba yake mdogo.

Kutokana na kitendo hicho, Hakimu Kashusha alisema hukumu hiyo imezingatia vipengele vyote vya msingi vya kisheria ikiwa ni pamoja na ushahidi wa kitabibu uliotolewa na daktari aliyemfanyia vipimo vyote mtoto pamoja na ushahidi uliotolewa na mama mzazi wa mtoto na mtoto mwenyewe. "Mahakama inamtia hatiani mshtakiwa kwa kumhukumu kifungo cha maisha jela baada ya kuridhishwa na ushahidi wa vielelezo uliotolewa na upande wa mashtaka pamoja na upande wa Jamhuri.

"Kufanya hivyo ni kosa kisheria na kwamba adhabu inayotolewa itakuwa fundisho kwa wengine wenye kufanya vitendo kama hivyo," alisema Hakimu Kashusha.

Awali, Mkuu wa Mashtaka Wilaya ya Masasi ambaye pia ni Wakili wa Serikali Mwandamizi Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali (DPP), Miraji Kajieuli, aliomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwa wengine wanaofanya vitendo vya kinyama kama hivyo.

Wakili Kajieuli alidai kuwa mshtakiwa alipaswa kuwa mlezi mwema kwa mtoto huyo na wengine walioko katika jamii lakini amegeuka na kuwa mnyama na kumlawiti mtoto jambo ambalo amemsababishia athari za kimwili na kisaikologia ambazo zitasalia kwake kwa miaka mingi atakayoishi duniani.

Mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea, hivyo aliiomba mahakama kumwachia huru kwa madai kuwa hajatenda kosa hilo na kwamba hukumu ya kifungo cha maisha jela itamwathiri kimaisha kwa vile yeye ni baba mwenye mke mmoja baada ya kufiwa na mke wake pili hivi karibun akiwa mahabusu. Pia alidai kuwa ana watoto watatu wote wanamtegemea kimaisha.

# Ma-RC wapewa kazi kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wakuu wa mikoa kufanya tathmini ya maeneo yanayofaa wananchi kuyatumia kwa ajili ya mazoezi ya viungo ili kukabiliana na wimbi la magonjwa yasiyo ya kuambukiza lililoko kwa sasa.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana bungeni katika kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu, wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Kunti Majala, ambaye alisema, Aprili 28, mwaka huu, (Majaliwa) akiongoza mbio kwa ajili ya kuchangia watoto wenye usonji, alielekeza daraja la Tanzanite litafungwa kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa tatu ili kupisha wananchi kufanya mazoezi.

"Je, serikali ina mkakati gani wa dhati kwa mikoa yote nchini, kuhakikisha suala la mazoezi linaendana na tamko lako ulilotoa Dar es Salaam,"alihoji.

Akijibu swali hilo, Majaliwa alisema, "Tumeona nchi nyingi zikifunga barabara ili kutoa fursa kwa wananchi kufanya mazoezi na shughuli za kijamii, tumeanza na Dar es salaam, nitoe wito kwa wakuu wa mikoa, kufanya tathmini maeneo yanayofaa kuwa viwanja na si kufunga barabara, ili wakabiliane na magonjwa hayo."

Alisema Aprili 28, mwaka huu, kulikuwa na mbio zilizolenga kuchangia fedha kwa ajili ya watoto wenye usonji na kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya, zilionyesha watanzania wengi wanakabiliwa na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

"Magonjwa haya yanatokana na mtindo wa kuishi, kutoshughulisha miili yetu



na tatizo hili limekuwa kubwa nchini, tumeanza kushuhudia watu au makundi yakianzisha mfumo wa kufanya mazoezi kwa pamoja, na Dar es Salaam wanaongeza kwa kuwa na vikundi vya mazoezi kila wilaya,"alisema.

Alisema kwa sasa jamii imeanza kupata uelewa wa umuhimu wa kufanya mazoezi na jukumu la serikali ni kuweka mazingira ya kuwezesha watanzania wafanye mazoezi ili kuepukana na magonjwa hayo.

"Kwa kuwa Jiji la Dar es salaam kuna makundi mengi na wanazagaa barabarani, tumeona kuna dalili wale wafanya mazoezi kupata ajali na msongamano wa magari, tumeona tuanze na Dar es Salaam kupanga siku moja ya Jumamosi kufanya mazoezi angalau kwa saa tatu, ili wakutane kwenye ufukwe wa bahari kupitia Daraja la Tanzanite wafanye mazoezi,"alisema.

Alisema uzinduzi wa mazoezi hayo utafanyika kesho ambapo atawaongoza wananchi kufanya mazoezi.

"Kwa kuwa tutaanza mazoezi katika eneo hili, vyombo vya usafiri vitakavyoruhusiwa kupita kwa muda huo ni magari ya wagonjwa, gari ya zimamoto, TANESCO na baiskeli.

Majaliwa aliagiza Jeshi la Polisi lisimamie hilo kusiwe na mwingiliano wa watu na magari.

## Wakulima korosho waomba bei elekezi

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

WAKULIMA wa korosho Masasi mkoani Mtwara wameiomba serikali kurejesha bei elekezi (BEI DIRA) ya zao hilo kama ilivyokuwa awali kwa madai kuwa wanunuzi wamekuwa wakiwapunja kwa kununua kwa bei ndogo, hivyo kutonufaika na jasho lao.

Hayo waliyasema jana wilayani hapa walipokuwa kwenye mikutano ya hadhara ya wakulima iliyoratibiwa na Mtandao wa Vikundi vya wakulima Tanzania (MVIWATA) iliyofanyika katika kata za Chiungutwa Temeke.

Wakulima hao walisema kitendo cha serikali kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) kuondoa bei elekezokatika korosho, kimesababisha kumkandamiza mkulima kupata maslahi madogo kwa vile hakuna bei halisi inayomfanya mnunuzi kununua zao hilo na kumletea tija mkulima.

Majidi Nampupa, mkulima wa kijiji cha Nangose Juu, kata ya Temeke, alisema kwa sasa wamekuwa na utaratibu wa wanunuzi kwenda katika minada ya korosho inayoendeshwa na CBT na kushindana bei na anayefikia bei ya juu kwiliko mwenzake, ndiye anapatiwa korosho.

Alisema mfumo huo bado haujamwezesha mkulima kuuza mazao yake kwa bei mzuri kwa kuwa mnunuzi anajipangia bei.

Grace Christopher, mkulima wa kijiji cha Chiungutwa alisema kutokana na hali hiyo, wakulima wa wilaya ya Masasi kwa niaba ya wakulima wote nchini, wanaiomba serikali kuona umuhimu wa kurejesha bei elekezi ya korosho ili kuwawezesha kunufaika na zao hilo.

Mkulima mwingine, Hamisi Jah, wa kijiji cha Chiungutwa, alisema iwapo kutakuwa na bei elekezi kwenye mfumo wa ununuzi wa korosho na mazao mengine, mnunuzi ataongozwa katika kununua zao hilo, hivyo kumfanya mkulima kuwa na uhakika wa kupata faida baada ya kuuza mazao yake.

„Tunaomba MVIWATA itusaidie kufikisha kilio chetu kuiomba serikali irejeshe bei dira ya korosho kwani tangu mfumo wa bei dira ulipoondolewa, mkulima hajanufaika kwa sababu mnunuzi anajipangia bei mwenyewe ya kununua mazao ya mkulima jambo ambalo si sawa," alisema Jah.

Pongezi Dadi, mkulima kutoka kijiji cha Nangose Juu, alisema kama serikali itasikia kilio cha wakulima cha kutaka irejeshwe bei dira katika korosho, ingeanzia kupangwa kwa Sh. 2,000 hadi 2,500 na kwamba mnunuzi anayetaka kununua kwa mkulima, aanzie kiwango hicho.

Mwenyekiti wa MVIWATA, Mustafa Mmeto, alisema wamesikia kilio cha wakulima na kwamba wanachukua maoni yao na watayafikisha kwenye vikao vya ngazi ya juu vya wadau wa korosho ili kufanyiwa kazi.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Kingine alichojiuliza ni kwa nini uchunguzi wa mwanzo wa madaktari useme kuwa tundu lililopo kichwani lilitokana na kuanguka baada ya kupata mshtuko wa moyo?

"Baada ya ndugu kuchachamaa, kwa nini uchunguzi wa pili ufanyike haraka na kukubali kuwa aliawa na si tena alianguka kwa kupata mshtuko wa moyo na kuanguka kwenye mtaro? Na kwa nini muuaji awe yeye wakati hajafanya kitendo hicho?" Akazidi kuwaza na kujiuliza.

Hii ilimpa picha kuwa yoyote aliye nyuma ya mpango huu atakuwa ni mtu ambaye hapaswi kuangalia kwa jicho jepesi. Ni mtu au watu waliojipanga, wenye uwezo mkubwa wa ushawishi, kwani wameweza hata kuingilia uchunguzi wa kidaktari, pamoja na wa polisi.

Kwa hili hata yeye mwenyewe alijiambia anapaswa kuwa makini, kwani licha ya kusakwa na polisi kwa ajili ya tuhuma hizi, lakini walio nyuma ya mpango huu wanaweza kumsaka na kumuua ili kupoteza kabisa ushaidi.

Kilichomuuma zaidi Kamal ni kuona maadui zake hao ambao hawajui wameweza kumfanya kuwa mbaya kwa jamii na ndugu za marehemu Mariamu, isipokuwa Teddy ambaye hata ukimuwekea bomu mdomoni hawezi kukubali kuwa mauaji na dada yake yamefanywa na yeye.

Alichokuwa anasubiri sasa ni kukutana na Teddy, wakati anamkabidhi vitu vyake muhimu alivyomuagiza amwambie ukweli aliokuwa nao na akitoka hapo aende kuwa balozi kwa ndugu zake kuwaaminisha kuwa hajafanya kitendo hicho. "Sijamuua mpenzi wangu. Siwezi kumuua Mariamu wangu." Akaongea kwa sauti bila kujijua.

Akaamua kwenda kulala kwenye gesti za bei ndogo mitaa yake Mwanyamala kwa Kopa, ambako alijua si rahisi kwa askari kufanya msako ili kupitisha siku kabla ya kuonana na Teddy.

Pamoja na kumuamini Teddy, lakini hakutaka kufanya kosa lolote la kiufundi ambalo lingeweza kumsababisha kukamatwa.

Katika kusoma vitabu vya kipelelezi na kutazama filamu zake, pamoja na kupendelea mambo hayo, alikutana na baadhi ya mbinu au miiko ya kazi hiyo.

Kwanza kabisa ni kutomuamini mtu yoyote. Hata kama ni baba, mama yako mzazi, au mke, mume, kwenye kazi hiyo hutakiwi kabisa kuwaamini. Ukifanya hivyo utakuwa umeepuka vitu vingine ambavyo vinaweza kuwa hatari kwako.




**Baada ya kuvamia mgahawa mmoja maeneo ya Kinondoni Studio, akanywa chai, chapati mbili na mayai mawili ya kukaanga. Alipanda daladala na kwenda kushuka kituo cha Kinondoni Kanisani, au wengine wanaita Morocco.**

Inawezekana hao wanaweza wasikudhuru moja kwa moja, lakini wakatumiwa bila kujua na maadui zako kukuangamiza.

Kwa maana hiyo hakutaka kumkaribisha Teddy, kwenye gesti ya Benson, kwa sababu hizo au zinazofanana na hizo. Hakutaka yoyote kujua anaishi wapi.

Ndiyo maana alimwambia wakutane kwenye kituo cha Magomeni Usalama. Tangu akiwa mdogo, Kamal alipenda sana kazi ya upelelezi, wengine wanaiita ya ushushushu. Lakini hakuweza kufanikiwa kutokana na kwamba elimu yake haikufika kule ambako alitakiwa kufika ili aweze kupata mafunzo hayo.

Badala yake akaishia kuwa fundi gereji, ingawa alikuwa ni fundi wa viwango vya juu mno.

Pamoja na hayo, kazi hiyo, lakini alifanya kazi kubwa ya kusoma vitabu vya kipelelezi vya kiswahili na kingereza. Kilichokuwa kinamfurahisha zaidi pamoja na mikasa mizito wanayokutana nao wapelelezi, lakini ni mbinu mbalimbali wanazotumia ili kukabiliana nazo.

Alikuwa akiziandika kwenye daftari lake. Mwenyewe alikuwa anapenda tu kuzitumia hata kwenye maisha yake ya kawaida. Kitu kingine ambacho aliona huwezi kuwa shushushu au mpelelezi kuwa na uwezo wa kupambana na adui. Alichofanya ni kwenda kwenye tempo ambazo zinafundisha michezo ya sanaa za mapigano. Alifanya hivyo baada ya saa za kazi na siku za mapumziko. Hakuna mtu wake wa karibu yoyote aliyejua hilo, hata marehemu mpenzi wake, Mariamu.

Aliiva kwa staili mbalimbali za mapigano kiasi kwamba akawa tishio. na mpaka leo ni mwanachama na mwalimu kwenye tempo hiyo iliyopo Kigamboni, ingawa bado anaendelea kuifanya kazi hiyo kwa siri. Kipindi chote hicho bado alikuwa akipenda kusoma vitabu vyake wa kipelelezi, pamoja na filamu za watu wa aina hiyo.

Baada ya kuvamia mgahawa mmoja maeneo ya Kinondoni Studio, akanywa chai, chapati mbili na mayai mawili ya kukaanga. Alipanda daladala na kwenda kushuka kituo cha Kinondoni Kanisani, au wengine wanaita Morocco.

Aliteremka taratibu na kupita nyuma ya Hospitali ya Magomeni na kutokea maeneo ya Usalama.

Itejensia yake ilimwambia asipite barabarani, hivyo akaamua kupita huko alikopita, alizunguka kwenye nyumba za NHC, kwani alikuwa anatafutwa kwa udi na uvumba na Jeshi la Polisi kwa kosa la mauaji ya mapenzi wake, Mariamu. Kisa, wivu wa mapenzi.

Kamal alitumia mbinu zile zile za kipelelezi kuwa unapotaka kwenda sehemu yoyote, iwe ya mualiko au kukutana na mtu kwa sababu za kikazi, au zinazofanana na hizo, au hata wewe mwenyewe umewaita kukutana nao, na una mashaka, basi usalama wako ni kuchelewa kwenye ahadi au kuwahi.

Ukiwahi unakuwa umejiwekea mazingira mazuri ya kumsoma au kuwasoma uliowaita, waliokuita au kukualika, na jitahidi wewe uwaone kabla wao hawajakuona, unaweza kujua nia yao ni nini. Kwa sababu wanaweza kufanya kitu ambacho ukahisi siyo watu wazuri kwako na wanakuita kwa ajili ya kukudhuru.

Kuchelewa pia kuna manufaa, kwani wanaokusaka kwa mabaya wanakuwa hawako kwenye hali ya kawaida, wameshaanza kuhamanika na kuulizana. Hili unaweza kulitambua pale utakapofika na kuanza kuwaona kabla wao hawajakuona. Lakini siyo siku zote inakuwa hivyo. wengine watu wazuri tu. Ila maisha ya kipelelezi siku zote ni kutia shaka kwa kila jambo, hata kama halina maana yoyote. Kwa sababu siku isiyo na jina linaweza kutokea jambo lolote lisilotarajiwa. Hapo ndipo mashushushu huonekana kama wachawi hivi kwani anaweza kuepuka jambo baya lililotarajiwa kumpata. Waswahili wanasema machale. Lakini mara nyingi wao hutumia mlango wa sita wa fahamu.

Kwa kawaida binadamu huwa ana hisia tano yaani kuona, kuonja, kusikia,kunusa, kuhisi kwa kutumia ngozi.

Watu wa itelejensia, mashushushu au wapelelezi hutumia hisia ya sita. Ni ipi?

Wataalam wanasema hisia ya sita wanakuwa nayo binadamu wa kawaida tu wenye hisia tano, lakini wao wanafundishwa, kujifunza au kufundwa namna ya kutumia akili waliyonayo kujiongeza, kuwa na uwezo hali ya juu ya kutambua, kuona, au kuhisi jambo ambalo si la kawaida ambalo kwa mtu wa kawaida hawezi kufanya hivyo. Inasemekana wapo waliozaliwa kuwa na uwezo huo wa kuwa na machale, lakini pia unaweza kujifunza. Kamal alikuwa mtu wa aina hiyo.

Alishawahi kuepuka balaa moja lililoelekea kumpata, alipoitwa na demu mmoja kule Bonyokwa.

Kama angekuwa mtu asiye na hisia ya sita, angeweza kupata fumanizi feki, kupigwa, kuibiwa, kujeruhiwa au kuuawa. Ilikuwaje?

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# TABORA UNITED FC SASA YAIPIGIA HESABU SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutolewa katika mashindano ya Kombe la FA, Tabora United FC imesema sasa 'macho' yote wanaelekezwa katika zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwamo dhidi ya Simba itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Tabora United ilifungwa mabao 3-0 na mabingwa hao watetezi wa michuano hiyo, Yanga ambao pia ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kikosi cha Tabora United kimebakia Dar es Salaam kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya kuivaa Simba.

Ofisa Habari wa Tabora United, Christina Mwagala, alisema timu hiyo inajiimarisha kuhakikisha hawapotezi pointi katika michezo ya sita iliyobakia iki kukamilisha msimu huu.

"Tumetolewa katika hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la FA, haikuwa malengo yetu tutolewe, mpango wetu ulikuwa ni kusonga mbele, lakini tumetolewa na Yanga, akili yetu yote sasa inarejea kwenye Ligi Kuu, ukiangalia hivi sasa tupo katika nafasi ya 15, siyo nafasi nzuri.

Mkononi tumebakisha michezo sita, hatutaki kupoteza pointi. Jumatatu tutacheza mechi ngumu dhidi ya Simba, ndiyo maana hatukutaka kuhamisha kambi, tumeendelea kusalia Dar es Salaam kwa ajili ya mazoezi, pamoja na kupanga mikakati ya kupata ushindi," alisema Mwagala.

Aliongeza kwa kuwahakikishia mashabiki wa timu hiyo Tabora United itabakia katika Ligi Kuu Tanzania Bara kutokana na mikakati waliyonayo kwenye michezo ya lala salama.

"Tabora United haitashuka daraja na wala kucheza mechi za mchujo, tunawaomba tushirikiane na kuipa sapoti timu yenu," Mwagalaaliongeza.

Mechi nyingine zilizobakia za Tabora United ni dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa Mei 9, mwaka huu kwenye utakaochezwa Uwanja wa Manungu Complex, Morogoro, Mashujaa FC (Mei 12- Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora), Mei 20, mwaka huu watakuwa hapo hapo nyumbani kuwakaribisha Ihefu FC.

Tabora itawafuata Yanga kwenye Uwanja wa Azam Complex, Mei 25, mwaka huu na itamaliza msimu huu ugenini Mei 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majaliwa dhidi ya Namungo.

Timu hiyo iko katika nafasi ya 15 kwenye msimamo ikiwa imecheza mechi 24, ikishinda mechi nne, sare 11 na imepoteza michezo tisa, ikivuna pointi 23.




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (katikati), akiwa na baadhi ya wanariadha wa Dodoma waliomtembelea ofisini kwake jana. Wanariadha hao watashiriki mbio za 'Amsha Amsha' zitakazofanyika leo kama sehemu ya maandalizi kuelekea msimu wa mwaka huu wa Betika Mbeya Tulia Marathon. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dodoma yajiweka sawa Mbeya Tulia Marathoni

**Mwandishi Wetu, DODOMA**

WANARIADHA wa jijini hapa watashiriki mbio maalumu maarufu Jogging kwa ajili ya kujiweka tayari kuelekea msimu mpya wa Betika Mbeya Tulia Marathoni utakaofanyika Mei 10 na 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Sokoine, Mbeya.

Wanariadha watakaofanya vizuri katika mbio hizo watakabidhiwa bendera ya mabingwa na ile ya Tulia Trust tayari kwenda kuchuana jijini Mbeya.

Ofisa Habari wa Betika, Rugambwa Juvenalius, alisema msimu huu wameongeza hamasa zaidi ikiwamo kuwagharamia wakimbiaji 460 kutoka mikoa mbalimbali.

Rugambwa alisema tayari 'Amsha Amsha' kuelekea katika mbio hiyo zimeanza ikiwamo mkoa wa Mtwara kufanya jogging kwa lengo la kujiweka fiti ili kushiriki Mbeya Tulia Marathoni msimu huu.

Alisema mbio hizo za awali pia zitafanyika Morogoro, Iringa, Rukwa na Dar es Salaam ambapo zitaongozwa na Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma (Mwana FA).

Mwakilishi wa Taasisi ya Tulia Trust, Leonard Mwinuka, alisema msimu huu hamasa ni kubwa na wanawakitarajia zaidi ya wakimbiaji 5,000 watashiriki.

"Wengi wanafanya marathoni, lakini Betika Mbeya Tulia Marathoni imejitofautisha na kuwa mbio pekee inayowapa fursa na wanariadha wa uwanjani kushindana. Kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, ili ni tukio kubwa na kama RT tunawashukuru waandaaji na wadhamini kwa kubuni huu utaratibu, tukiendelea hivi tutapanua wigo na kuibua vipaji vya mbio za uwanjani," alisema Makamu wa Rais wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), William Kallaghe.

## Kado afurahia kuipandisha Pamba

**Na Somoe Ng'itu**

KIPA chaguo la kwanza la Pamba Jiji FC, Shabani Kado, amesema anafurahia kuwa sehemu ya wachezaji waliosaidia kuirejesha timu hiyo katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Pamba Jiji itashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Ligi ya Championship msimu huu, ikiwa nyuma ya vinara, KenGold ya Mbeya ambao ndio mabingwa wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kado, alisema walicheza mechi zote kwa kujituma na hawakudharau wapinzani wao.

"Ndoto inakuwa ndoto mpaka pale utakapoamua kuifanya iwe kweli," alisema Kado, kipa wa zamani wa Mtibwa Sugar ya Morogoro na Simba ya Dar es Salaam.

Biashara United ya Mara na Mbeya Kwanza zenyewe zinasubiri kucheza mechi za mtoano na timu kutoka katika Ligi Kuu Tanzania Bara, ili kujihakikishia nafasi ya kupanda daraja au kubakia kwenye Ligi ya Championship kwa mara nyingine.

## Kipa Ihefu afunguka siri iliyowabeba FA

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya timu yake kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA, kipa chaguo la kwanza wa Ihefu (Singida Black Stars), Abubakary Khomeiny, amesema siri ya timu yao kusonga mbele ni kujituma na ushirikiano.

Ihefu imesonga mbele katika mashindano ya Kombe ka Fa baada ya kuufunga Mashujaa FC penalti 4-3 kutokana na kutoka suluhu katika dakika 90 ya kawaida.

Khomeiny alipangua penalti mbili kati ya tano zilizopigwa na wachezaji wa Mashujaa na hivyo kuibeba timu yake katika mashindano hayo ambayo bingwa ataiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Khomeiny alisema wachezaji wa timu hiyo wanajituma zaidi mazoezini kwa ajili ya kufanya vizuri na pia wanajitahidi kufuata vyema maelekezo ya makocha wao.

"Mashindano haya ni magumu, lakini tunamshukuru Mungu tumefanya vizuri, tumekuwa tunawasikiliza sana makocha wetu kwa kila jambo, tunajua michuano hii ni migumu na pia kuna ligi inatusubiri, ni lazima tupambane," alisema kipa huyo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MICHAEL OLISE ATAKIWA MAN**

KLABU ya Manchester United ipo mbioni kumsajili kiungo wa kati wa Crystal Palace na Ufaransa chini ya umri wa miaka 21, Michael Olise. ***(ESPN)***

**GREENWOOD AWANIWA JUVE**

JUVENTUS inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mashambuliaji wa Manchester United na England, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22, ambaye yuko kwa mkopo katika klabu ya Getafe ya Hispania. ***(i Sport)***

**XAVI AMTAKA SILVA**

KOCHA wa Barcelona, Xavi ameiambia klabu hiyo kwamba anamtaka kiungo wa kati wa Manchester City na Ureno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 29, lakini Bayern Munich pia wanamtaka. ***(Sport)***

**IHEANACHO ATAKIWA VILLA**

ASTON Villa wanataka kumsajili shambuliaji wa Leicester na Nigeria Kelechi Iheanacho mwenye miaka 27, kama mshambuliaji msaidizi wa mchezaji wa kimataifa wa England, Ollie Watkins, 28. ***(Football Insider)***

**DI MARIA KUTUA MIAMI**

KLABU ya Inter Miami imeanza mazungumzo na winga wa Benfica na Argentina mwenye umri wa miaka 36, Angel di Maria. (ESPN)

**SZCZESNY ATAKIWA CHELSEA**

CHELSEA inafikiria kumnunua mlinda lango wa Poland, Wojciech Szczesny mwenye umri wa miaka 34 ambaye sasa anachezea Juventus. ***(Tutto Juve)***

**TOSIN AWA LULU ENGLAND**

CHELSEA imeungana na Newcastle United kuulizia hali ya mchezaji wa zamani wa kimataifa wa England, Tosin Adarabioyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye ataondoka Fulham kama mchezaji huru msimu huu wa joto. ***(Fabrizio Romano)***

**MAATSEN ACHUNGUZWA**

KLABU ya Manchester City ilikuwa miongoni mwa timu zilizomchunguza beki wa Borussia Dortmund Mholanzi Ian Maatsen mwenye miaka 22. ***(TBR Football)***

**JESUS KUPIGANIA NAMBA**

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 27, yuko tayari kupigania nafasi yake katika klabu ya Arsenal huku kukiwa na tetesi zinazoashiria mchezji huyo anaweza kuondoka majira ya kiangazi. ***(Sun)***

**O'HARE ATAKIWA LEICESTER**

KLABU ya Leicester City ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Coventry City, Callum O'Hare mwenye umri wa miaka 26. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DE ZERBI ANUKIA BAYERN MUNICH

Jina la kocha huyo limeibuka kwa kasi katika kipindi hiki ambacho...

**MUNICH, Ujerumani**

JINA la Kocha Mkuu wa Klabu ya Brighton & Hove Albion, Roberto De Zerbi limeibuka katika kinyang'anyiro cha kuwania nafasi ya Kocha Mkuu wa Mabingwa wa zamani wa Ujerumani Bayern Munich.

Uongozi wa Bayern Munich kwa sasa upo katika heka heka za kusaka Kocha Mkuu mpya wa kikosi chao, baada ya kufikia makubaliano ya kusitisha mkataba na kocha wao wa sasa Thomas Tuchel atakayeondoka mwishoni mwa msimu huu.

De Zerbi ambaye alikuwa hatajwi katika kinyang'anyiro hicho, jina lake limeibuliwa na Gazeti la Daily Mail, ikielezwa anajipanga kuondoka Brighton mwishoni mwa msimu huu, ili kufanikisha mpango wa kuelekea mjini Munich, Ujerumani.

Gazeti la Daily Mail limeripoti kuwa, Kocha huyo kutoka nchini Italia amedokeza kwamba anaweza kuondoka katika klabu hiyo wakati wa majira ya joto.

Gazeti hilo limeandika: "Kocha wa Ligi ya England ameibuka kuwa kocha anayepewa nafasi kubwa ya kukinoa kikosi cha FC Bayern Munich msimu ujao.

"De Zerbi aliibua wasiwasi juu ya mustakabali wake mwanzoni mwa msimu huu 2023/24, na kukataa kujitoa kwa 'Seagulls' huku akikiri alihitaji kuhakikisha anakuwa na 'maono' sawa na klabu.

Kabla ya kuhusishwa na Bavaria hao Kocha huyo aliwahi kuhusishwa na mpango wa kuhamia Liverpool na Barcelona, lakini klabu hizo zinaonekana kusitisha mpango huo, huku Arne Slot akikaribia kuteuliwa kuwa Kocha Mkuu wa Wekundu hao na Xavi akiamua kusalia Camp Nou.

"De Zerbi mwenye umri wa miaka 44, anaweza kuondoka wakati wa majira ya joto, akiwa na fursa ya kuchukua jukumu la kukinoa kikosi cha moja ya klabu kubwa barani Ulaya."

# SANCHO KUUZWA JUMLA DORTMUND

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inatarajia Jadon Sancho kuondoka katika klabu hiyo msimu wa joto bila kujali kama kocha Erik ten Hag atasalia kuiongoza au la, chanzo kiliiambia ESPN.

Sancho alitolewa kwa mkopo kwa klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund Januari mwaka huu kufuatia kutofautiana hadharani na Ten Hag.

Mustakabali wa Mholanzi huyo kama kocha upo shakani baada ya msimu mbaya, lakini chanzo kiliiambia ESPN kwamba United bado inapanga kuondoka kwa Sancho.

United haitarajiwi kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wa Ten Hag hadi baada ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester City Mei 25.

Sancho ana makubaliano na Borussia Dortmund hadi mwisho wa msimu huu, lakini bila chaguo au wajibu wa kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu.

Timu hiyo ya Bundesliga ingependa kumbakiza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, lakini vyanzo vimeiambia ESPN kwamba hawawezi kuendana na mshahara wake.

Mkopo wa pili wa msimu wa 2024-25 unawezekana, lakini upendeleo wa United ni uhamisho wa kudumu.

Sancho, ambaye yuko chini ya mkataba hadi 2026, alijiunga na United kwa kitita cha pauni milioni 73 mwaka 2021 na klabu ingependa kurudisha ada nyingi iwezekanavyo.



Mchezaji huyo wa kimataifa wa England ameichezea Dortmund wakati wa mbio zao za Ligi ya Mabingwa na ndiye mchezaji bora zaidi katika ushindi wa 1-0 dhidi ya PSG katika mchezo wa nusu fainali ya kwanza Jumatano.

## Manchester City yajuta kuondoka kwa Gundogan

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City imeripotiwa 'kujuta' kumruhusu Ilkay Gundogan kuondoka katika klabu hiyo msimu uliopita wa joto, wakimtazama kiungo huyo akisajiliwa na Barcelona kwa uhamisho wa bure.

Gundogan na wakala wake waliacha chaguzi zao 'wazi' mara tu mchezaji huyo alipoingia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake na City na kuruhusiwa kufanya mazungumzo kwa uhuru na klabu nyingine.

Mazungumzo na Barcelona yalikuwa tayari yamefanyika mwishoni mwa Machi, ambayo City walikuwa wanafahamu na walikuwa tayari kumwacha mchezaji huyo kuamua kubaki au kuondoka bila kulazimisha suala hilo.

Kama ilivyoripotiwa na 90min wakati huo, City walikuwa bado wanatumaini kwamba Gundogan angesaini mkataba mpya Aprili. Lakini alikuwa karibu kufikia makubaliano na Barcelona na hakushawishiwa kabisa kutokwenda.

Hata hivyo, kuondoka kwake Etihad na uamuzi wa kujiunga na Barcelona ulitangazwa baada ya kuwa nahodha wa City wakati wakitwaa mataji matatu ya Ligi Kuu, Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Msimu wa 2023/24, kikosi cha Pep Guardiola kimeshindwa kutamba kwenye Ligi ya Mabingwa, lakini bado kinabakia kuwa na uwezekano wa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya England na watamenyana na Manchester United kwenye fainali ya Kombe la FA.

Gundogan alionekana kuwa muhimu katika kuifanya City kuwa juu ya mstari wakati huu mwaka jana, hasa pale Wembley alipofunga mabao yote mawili katika ushindi wa 2-1 - likiwemo la haraka zaidi katika historia ya fainali ya Kombe la FA.

Sasa, Mundo Deportivo inaripoti kwamba Guardiola anakosa uwepo wa nahodha wake wa zamani, aina yake ya uchezaji na mchango wake kwa ujumla.

Wachezaji mbadala kama Mateo Kovacic na Mathues Nunes hawajaziba pengo kabisa.



## Pochettino atema nyongo Chelsea

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino hakuficha furaha yake baada ya timu yake kushinda 2-0 dhidi ya Tottenham Hotspur, akisisitiza ushindi huo umethibitisha kile anachoweza kufanya akipewa muda wa kutosha wa kupata mawazo yake.

Pochettino amekuwa chini ya shinikizo kubwa msimu wote baada ya kushindwa kuhamasisha mabadiliko ya mara moja huko Chelsea, lakini jibu la kuvutia la kuteswa na Arsenal mwezi uliopita liliendelea na ushindi mzuri dhidi ya waajiri wake wa zamani Alhamisi.

Baada ya mchezo huo, Pochettino alikiri kuwa ni "vigumu" kuchunguzwa kila mara na alikiri kuwa hajui kama atapata muda unaohitajika kuendelea na kazi yake.

"Nadhani inatosha," aliambia Sky Sports alipoulizwa kuhusu uvumi huo.

"Makocha wote wanahitaji muda wa kutafsiri mawazo yao na falsafa zao. Zaidi wakati timu iko kama kikosi hiki. Tunahitaji kuwa na muda, sio uamuzi wangu.

"Ni vigumu kuona kila wiki ninachunguzwa na ninahukumiwa. Lakini sio uamuzi wangu kuwa hapa au kutokuwa hapa. Ikiwa tunataka historia ya Chelsea, nadhani ni kazi kubwa kufanya. Tutaona kama tuna muda wa kuwa hivi.

"Hisia zangu ni kwamba mimi niko hivyo, ninajivunia kwamba hawa watu wote, kikosi chote tulichonacho, wachezaji 25 hadi 27 tunawatakia mema na hadi siku ya mwisho tutajaribu kuwasaidia."

Akiendelea na majibu yake makali, Pochettino aliendelea kusisitiza uchezaji wa Chelsea ulikuwa ushahidi kwamba kutegemea "majina makubwa" sio njia ya kusonga mbele.



"Watu wanaamini kwamba kwa sababu mchezaji ni jina, anapaswa kucheza, hata kama hayuko katika kiwango au ubora wake," Pochettino alisema.

"Nadhani timu, tangu mwanzo wa msimu, ilipata shida nyingi, ambazo wakati mwingine majina yalikuwepo, lakini sio katika kiwango chetu bora.

"Hatukuwahi kupata imani kwamba tulihitaji kucheza kwa njia hii. Kulikuwa na malengo au malengo mengi ya mtu binafsi mbele ya timu.

"Leo ilikuwa uteuzi rahisi wa timu kwetu, lakini wakati huo huo, tulionesha kwa kila mtu kuwa mpira wa miguu sio wa majina. Ni juu ya kuwa na ushindani, juu ya tabia kama timu."

# AZAM YAPANIA MAKUBWA MSIMU UJAO MICHUANO CAF

**Na Faustine Feliciane**

HAWATAKI utani, ndio kinachoonekana ndani ya Azam FC ambayo imejipanga kujiimarisha kwa kufanya usajili ,mkubwa' kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki.

Baada ya kuhusishwa kuweka mezani ofa kuhitaji huduma ya wachezaji wawili wa Simba, Aishi Manula na Kibu Denis, Azam inatajwa imeanza kuwinda sahihi ya beki wa Yanga, Kibwana Shomari.

Taarifa zilizopatikana jijini, Dar es Salaam zinasema Azam imeanza mchakato wa kumsajili Kibwana na mazungumzo yamefikia katika hatua nzuri.

Chanzo hicho kilisema Azam inaamini ikimpata beki huyo wa pembeni itafanikiwa kuongeza nguvu kikosi chake ili kifikie malengo. „Uongozi unafuatilia kwa karibu suala la Kibwana, inafahamika bado hajasaini mkataba mpya na Yanga, na kama watachelewa inawezekana msimu ujao akachezea Azam.

Tunataka Azam FC ya msimu ujao iwe ya tofauti sana na ndio maana mipango imeanza mapema kukisuka kikosi chetu, lakini pia kuna uwezekano mkubwa wa kushiriki mashindano ya kimataifa, tunataka kufanya vizuri kwa sababu mara nyingi tumekuwa tukiishia hatua za awali," kilisema chanzo chetu kutoka kwa klabu hiyo ya Chamazi.

Hata hivyo kuhusu usajili wa Kibwana na nyota wengine, Msemaji wa Yanga, Ali Kamwe, alisema uongozi wa timu hiyo unaendelea na mazungumzo kuhakikisha inawabakisha wachezaji wote inaowahitaji na ambao mikataba yao inaelekea ukingoni.

„Niwatoe hofu mashabiki na wanachama wa Yanga, uongozi wetu upo makini sana, hakuna mchezaji tunayemhitaji ataondoka Yanga, wale wote ambao tunaona wanahitajika ndani ya klabu watabaki na tutakuwa nao msimu ujao," alisema Kamwe.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Saidi Mtanda (kushoto), akimkabidhi cheti cha shukrani Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa Pamba Jiji FC ya jijini Mwanza, Evarist Hagila, kutokana na kusaidia timu hiyo kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara. **PICHA: MTANDAO**

# Aziz Ki 'hatari' mabao mashuti ya mbali Bara

**Na Adam Fungamwango**

KINARA wa mabao wa Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, Stephane Aziz Ki, anaongoza kwa kufunga mabao kwa mashuti ya mbali katika ligi hiyo inayoelekea ukingoni.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Bodi ya Ligi Kuu jana, pamoja na za dawati la michezo la Nipashe, zinaonyesha raia huyo wa Burkina Faso huyo amefunga mabao matano akiwa nje ya boksi mpaka sasa.

Aziz Ki, ambaye amepachika mabao 15 mpaka sasa katika ligi hiyo, ni mmoja wa wachezaji ambao ni hatari kwa kupiga mashuti ya mbali, akiwa anakokota mpira, au kwenye mikwaju ya faulo.

Wakati Aziz Ki, aliongoza kwa mabao ya mashuti ya mbali, kiungo mshambuliaji mwingine wa Ihefu FC, raia wa Togo, Marouf Tchakei, anafuatia akiwa na mabao matatu ambayo ameyapachika akiwa nje ya boksi.

Wachezaji watano wanakamata nafasi ya tatu kwa kukwamisha wavuni mabao kwa mashuti ya mbali, nao ni Edwin Barua wa Simba, moja akilifunga akiwa kwenye timu yake hiyo mpya na lingine alipotoka, Prisons, pamoja na Clatous Chama, wote wakitokea Wekundu Msimbazi, wakiwa wamepachika mabao mawili, kila mmoja.

Wengine waliopachika mabao mawili, ni Valentino Mashaka na Tariq Seif, wote wa Geita Gold, Kipre Junior na Azam FC.

## Kocha Kipanga FC alilia 'ukuta'

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya timu yake kupoteza mechi dhidi ya KVZ, Kocha Msaidizi wa Kipanga FC, Adam Ali, alisema kikosi chao hakikuwa na bahati katika mechi hiyo ambayo walifungwa bao 1-0 na vinara wa Ligi Kuu Zanzibar.

Ali aliliambia gazeti hili kikosi chake kilifanya maandalizi mazuri na kilionyesha kiwango bora ingawa hawakufanikiwa kuvuna alama tatu muhimu.

„Wachezaji wangu walicheza vizuri na walikuwa na utulivu mkubwa katika kipindi chote cha mchezo, hata wapinzani walipopata goli, timu haikurudi nyuma kiuchezaji, makosa madogo madogo tuliyoyabaini tutayafanyia kazi," alisema Ali.

Aliongeza wanatambua ugumu na ushindani wa michezo iliyobakia hivyo wanahitaji kuongeza umakini zaidi ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na hatimaye kufikia malengo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar inayoshirikisha timu 16, Kipanga ipo kwenye nafasi ya sita ikiwa na pointi 31 kibindoni.

## KenGold yaanza mipango mapema

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa klabu ya KenGold ni kama wameshtuka kwa kujipanga kuanza mipango ya usajili mapema ili kujiweka imara.

Akizungumza na gazeti hili, Mkurugenzi wa KenGold, Keneth Mwambungu, amesema wametumia nguvu kubwa na kupambana kupanda daraja, hivyo hawataki kuona wanashuka haraka au kushiriki Ligi Kuu kwa msimu mmoja.


Mwambungu alisema wameanza mikakati ya kukiimarisha kikosi chao ili kutoa ushindani katika kila mechi ya Ligi Kuu watakayocheza.

"Ni ngumu kusema tutachukua ubingwa msimu wa kwanza tu wa Ligi Kuu, lakini tunataka kuonyesha ushindani na hata mwishoni mwa ligi tuwe na uhakika wa kuendelea kubakia," alisema Mwambungu. Aliongeza licha ya kuwa na kikosi kizuri ambacho kimewapandisha daraja, wamepanga kukiimarisha zaidi pamoja na benchi la ufundi hili kwenda na kasi ya Ligi Kuu.

Bosi huyo aliweka wazi licha ya kutamani kutumia Uwanja wa Chunya, itawabidi baadhi ya mechi za awali watumie Uwanja wa Sokine jijini, Mbeya wakati wakikamilisha ukarabati ambayo utapelekea utimize vigezo.

Michezo
Jumamosi Mei 4, 2024
Nipashe

De Zerbi anukia Bayern Munich UKURASA 21



# SIMBA KUTEMA NYOTA TISA

## ●●●Yaichapa Mtibwa na kuendelea 'kuichimbia'...

**Saada Akida na Faustine Feliciane**

HUKU ikipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana, Wekundu wa Msimbazi inajipanga kutema wachezaji tisa na wengine ikitarajia kuwatoa kwa mkopo, imeelezwa.

Kwa mujibu wa habari zilizopatikana jijini zinasema wachezaji watakaotemwa wapo wa zamani na baadhi ni nyota wapya waliosajiliwa hivi karibuni lakini wameshindwa kufikia malengo na wanatakiwa kupisha wengine ili kuisaidia timu hiyo.

Chanzo hicho kilitajawa kati ya watakaotemwa yupo kipa mmoja, mabeki wawili, viungo wawili, mawinga wawili na washambuliaji wawili.

„Tayari viongozi wa klabu wameshaanza kutafuta wachezaji wenye ubora wa hali ya juu kwa ajili ya kusajiliwa na hapa ninapozungumza, yapo majina matatu mezani ambayo mchakato wake umeshafanyiwa kazi," kilisema chanzo chetu.

Kwa sasa ofa rasmi ya Kibu itawasilishwa katika kikao na nyota huyo pamoja na viongozi kitakachofanyika wiki ijayo. Tutazungumzia mustakabali wake, pia kuangalia hatima ya wachezaji wengine ambao mikataba yao imefikia tamati," kiliongeza chanzo chetu.

Kilisema pia uamuzi wa nani atabakia na nani ataondoka, unatarajiwa kujadiliwa kwa sababu wanataka kukamilisha mchakato wa asilimia 80 ya usajili kabla ya msimu huu haujamalizika.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema klabu hiyo inatarajia kufanya mchakato wa usajili kwa weledi kwa sababu wanahitaji kurejea katika ushindani.

Ahmed alisema wanachokifanya sasa viongozi wa klabu hiyo ni kuwabakisha wachezaji bora na wenye ‚moyo' wa kuitumikia timu wakati wote.

Aliongeza licha ya timu yetu kusemekana ni mbovu lakini ndio timu inayoongoza wachezaji wake kutakiwa na klabu nyingine za ndani na nje ya Tanzania.

„Ni dhahiri tuna kikosi chenye wachezaji bora. Hatujapata matokeo mazuri msimu huu lakini haiondoi ukweli wachezaji wetu ni bora sana, ndio maana wanatajwa sana sokoni," meneja huyo aliongeza.

Mabao mawili yaliyofungwa katika kila kipindi yalizidi kuiweka pabaya Mtibwa Sugar katika mbio za kujinusuru kushuka daraja huku ushindi huo ukiifanya Simba ifikishe pointi 50, lakini wakisalia pale pale katika nafasi ya tatu kwenye msimamo huo wa Ligi Kuu Bara.

Simba ilianza kuandika bao la kwanza dakika ya 34 kupitia, Fred Michael aliyeunganisha kwa kichwa krosi ya Saido Ntibanzokiza huku goli la pili likipatikana dakika ya 64 kwa kufungwa na mtokea benchi, Salehe Karabaka aliyeingia kuchukua nafasi ya Willy Onana.

Karabaka alifunga bao hilo baada ya kuunganisha pasi safi iliyopigwa na Muzamiru Yassin na ilikaribia kupata bao la tatu lakini mpira wa faulo uliopigwa na Edwin Balua uligonga mwamba na kutoka nje.



Mshambul[illegible] wa Simba, Fredy Michael (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Mtibwa Sugar, Tiote katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana. Simba ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Musonda, Okrah waivuruga Yanga SC

**Na Saada Akida**

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wakiusogelea ubingwa wa msimu huu, nyota wake wawili, Kennedy Musonda na Agustino Okrah, wamekuwa katika sintofahamu ya kubakia au kutemwa ndani ya kikosi cha timu hiyo.

Yanga ambayo imetinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA, iko katika nafasi nzuri ya kutetea ubingwa wa michuano hiyo.

Taarifa zilizopatikana kutoka ndani ya Yanga zinasema bado uongozi haujafikia uamuzi wa nani ataondoka kati ya Musonda na Okrah.

Chanzo hicho kilisema hatua hiyo ya kuachwa kwa mchezaji mmojawapo imetokana na mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, ya kutaka kupunguza mawinga na kuongeza washambuliaji.

Habari zaidi zinasema pia Yanga huenda ikawapa ‚Thank You' wachezaji wake mbalimbali wakiwamo Joyce Lomalisa, Skudu Makudubela na Bakari Mwamnyeto ambaye amepata timu huko Afrika Kusini.

„Kazi kubwa ipo kwa Skudu na Musonda mmoja wapo anatakiwa kutemwa ila hadi sasa viongozi wanaumiza kichwa kwa sababu ya kuhakikisha wanaongeza mtu kulingana na mapendekezo ya kocha," alisema mtoa habari huyo.

Aliongeza Yanga imeshaanza mazungumzo na wachezaji sita wa kigeni huku Rais, Hersi Said, akitarajia kwenda Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), kukamilisha mchakato wa kuwapata baadhi ya nyota ambao wako nchini humo.

"Kati ya hao sita yupo Prince Dube ambaye ameshasaini mkataba wa miaka miwili, anatatajiwa kulipwa mshahara wa Sh. milioni 15 kwa mwezi," chanzo hicho kiliongeza.

Akizungumza na gazeti hili, Lomalisa aliweka wazi mkataba wake unakaribia kufikia tamati baada ya kubakiza mwezi mmoja.

"Napenda kubakia kuitumikia Yanga, lakini hawajanitafuta kwa ajili ya kuzungumzia mkataba mpya, nimebakiza mwezi mmoja tu, hakuna mazungumzo, kama kuna timu zinanihitaji huduma yangu zinatakiwa kuwasiliana na meneja wangu," alisema nyota huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042